SUPA JACKPOT
TZS. 1,139,859,317
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**CHADEMA** watosa tena mkutano wa Msajili wa Vyama

UKURASA 3



**VAN DIJK NAHODHA MPYA LIVERPOOL**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatano Agosti 2, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581390

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


LIKE & FOLLOW US


# Waliopandikizwa uume wakiri 'heshima' imerudi

**HOSPITALI** yatamba kupata suluhisho tatizo la nguvu za kiume... *Endelea Ukurasa wa 15*

## Mpango aonya lugha chafu dhidi ya Samia

UKURASA 2




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Asas, Ahmed Abri kuhusu masuala mbalimbali ya ufugaji, kabla ya kufungua maonyesho ya kitaifa ya kilimo ya Nanenane, katika viwanja vya John Mwakangale, mkoani Mbeya jana. **PICHA: OMR**

UKURASA WA 4

### WAZIRI AAGIZA MHANDISI WA HALMASHAURI ACHUKULIWE HATUA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, amemwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mkoani Kiliman-

UKURASA WA 5

### MADELEKA AZIDI KUSOTA MAHABUSU



MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imetupilia mbali ombi la kupatiwa dhamana Wakili wa Kujitegemea Peter Madeleka, hivyo...

## 'Panya road' wadaiwa kuua mhitimu kidato cha nne kikatili

UKURASA 2

**MICHEZO** ROBERTINHO AZITISHA TIMU LIGI KUU, CAF UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Mafundi wakitoa mabomba ya maji ili kupisha upanuzi wa barabara eneo la Goba Centre, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mpango aonya lugha chafu dhidi ya Samia

**Nebart Msokwa na Ashton Balaigwa,** MBEYA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewaonya watu wanaotumia uhuru wa kujieleza kumtolea lugha za matusi Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi wengine kuhusu azma ya serikali kuwekeza katika bandari.

Dk. Mpango alitoa onyo hilo jana wakati akifungua rasmi maonyesho ya kilimo, ufugaji na uvuvi, maarufu kama Nanenane yanayofanyika kitaifa katika viwanja vya John Mwakangale, mjini hapa yakihusisha mikoa ya Kanda za Nyanda za Juu Kusini. Alisema uvumilivu dhidi ya kauli hizo za matusi umefika mwisho.

"Rais wetu ameonyesha uvumilivu na ukomavu wa hali ya juu sana kuhusu wanaotumia fursa ya uhuru wa kuongea na alifungua uwanja wa kisiasa ili kufanya siasa za kistaarabu. Matusi si utamaduni wa Mtanzania. Ninawasihi kuacha mara moja. Tumeshafanya busara kubwa, nawasihi kiungwana waache," alisema.

Dk Mpango alisema badala ya kujadili hoja, watu hao wamekuwa wakitoa matusi na kutoka nje ya ajenda iliyopo na kwa kuwa tayari Watanzania wameshawaelewa nia yao, sasa wajadili maendeleo ya mama Tanzania.

"Tunataka Tanzania ya amani na tunataka Tanzania iendelee haraka ili watoto wetu tuwafundishe katika maadili ya uzalendo wa mama Tanzania. Kwa hiyo nawasihi tena na ninasisitiza maana wengine wanasema naona Makamu amenyamaza. Ni busara kubwa inatumika kwa hiyo nawambia wasitupeleke huko," alisema Dk. Mpango.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, kwa sasa Watanzania wanaona mambo yanayoendelea nchi jirani kumekuwa na vurugu barabarani na hawana muda wa kuzungumzia maendeleo ya wananchi, hivyo alisisitiza serikali haitaki kwenda huko kama nchi jirani.

**BASHE ASHANGAA**

Awali, Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe, alimweleza Dk. Mpango kuwa anashangazwa na uungwana ulioonyeshwa na Rais Samia kwa kukaa kimya na kutumia busara dhidi ya wanaotoa lugha za hovyo.

Kuhusu maonyesho ya Nanenane, Dk. Mpango alimwagiza Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na wakuu wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, kudhibiti uingizwaji wa makundi ya mifugo kwa kuwa inachangia uharibifu wa mazingira.

Dk. Mpango alisema uingizwaji holela wa mifugo kwenye mikoa hiyo unachangia ongezeko la migogoro ya wakulima na wafugaji na migogoro ya wafugaji na hifadhi za taifa.

Aliwataka viongozi hao kupanga matumizi bora ya ardhi kwa kuhakikisha maeneo ya malisho yanatengwa na washirikiane na wafugaji kujenga malambo kwa ajili ya kunyweshea mifugo, ili kuwasaidia kuacha kuhamahama na mifugo.

"Uvamizi huo wa makundi ya mifugo umeanza kusababisha wanyama kama tembo kukimbia kwenye maeneo yao na kuingia kwenye makazi ya watu ambako wanaharibu mazao na kuua watu. Kwa hiyo lazima mdhibiti uingizwaji wa mifugo hii," alisema Dk. Mpango.

Pia aliwataka viongozi hao kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu ufugaji wa mifugo michache na kuuza ziada ili idadi ya mifugo inayokuwepo iendane na ukubwa wa maeneo.

**TAHADHARI WAKULIMA**

Katika hatua nyingine, Dk. Mpango aliwataka wakulima kutouza chakula chote na badala yake wauze ziada ili kuhakikisha kunakuwapo na usalama wa chakula katika ngazi ya kaya.

Aidha, aliagiza Wizara ya Kilimo na Wizara ya Fedha kushirikiana kuunda mfuko wa maendeleo ya kilimo utakaowawezesha wakulima kupata mikopo yenye riba nafuu pamoja na taasisi za kifedha kupunguza riba.

Pia aliagiza Wizara ya Kilimo kupima maeneo yote ya utafiti na uzalishaji wa mbegu na kuyalinda ili yasivamiwe na wananchi pamoja na kuhakikisha uzalishaji wa mbegu unakuwa endelevu.

**MABORESHO KILIMO**

Waziri Bashe alisema serikali inaendelea kuboresha sekta ya kilimo kwa kuhakikisha inawatengenezea wakulima mazingira rafiki ya uzalishaji wa mazao mbalimbali hasa kuboresha utoaji wa elimu.

Alisema wizara hiyo kwa mwaka huu wa fedha, imeongeza bajeti kutoka Sh. bilioni 290 ya mwaka uliopita mpaka zaidi ya Sh. bilioni 900 na kwamba ongezeko hilo ni kwa ajili ya kuimarisha maeneo mbalimbali.

Aliyataja maeneo ambayo wanaboresha kuwa ni utafiti, kuboresha kilimo cha umwagiliaji kwa kuchimba mabwawa na visima pamoja na ruzuku ya pembejeo za kilimo.

"Mwaka huu wa fedha tumepanga kuanza na ujenzi wa mabwawa 100 nchi nzima kwa ajili ya kuboresha kilimo cha umwagiliaji. Lakini pia tunapanga kuchima zaidi ya visima 600 nchi nzima," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wakuu wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema mikoa inachangia kuimarisha usalama wa chakula nchini kutokana na kuwa na kiwango kikubwa cha uzalishaji wa mazao ya chakula.

Homera alisema katika msimu uliopita wa kilimo, mikoa hiyo ilizalisha zaidi ya tani milioni 11 za mazao ya chakula huku mahitaji ya chakula ikiwa ni tani milioni mbili, hivyo kuwa na ziada ya chakula ya tani milioni tisa.

Pia alisema mikoa hiyo ilizalisha zaidi ya tani 600,000 za mazao ya biashara na kwamba baadhi yanazalishwa katika mikoa yote na mengine kwenye baadhi ya mikoa.

Maonyesho ya wakulima yenye hadhi ya kimataifa, yanafanyika kwa mara ya kwanza mkoani Mbeya na zaidi ya mataifa 30 yanashiriki ikiwamo India na nchi za ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

## 'Panya road' wadaiwa kuua mhitimu kidato cha IV kikatili

**Na Elizabeth Zaya**

KUNDI la vijana wanaodhaniwa wahalifu wa mitaani Dar es Salaam, maarufu 'panya road', limemvamia mhitimu wa kidato cha nne, Hadija Hamisi (18), na kumchoma na kitu chenye ncha kali kifuani na kumsababishia kifo.

Kundi hilo la vijana wanaokadiriwa kuwa 30, linadaiwa pia kujeruhi watu wengine wanane kwa kuwachoma na vitu vyenye ncha kali katika maeneo tofauti ya miili yao huko Vingunguti, wilayani Ilala jijini Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na Nipashe jana, mama wa kijana huyo , Anna Mhawe alisema kundi la vijana hao lilipita katika eneo analofanyia biashara, likitoka katika maziko ya mwenzao na kufanya vurugu za kuwajeruhi watu.

"Juzi (jana), tukiwa dukani kulitokea vurugu ambazo zilisababishwa na 'panya road', walipita katika eneo letu Vingunguti ninakofanyia biashara, ilikuwa saa tatu usiku, wakaleta vurugu kubwa na kujeruhi watu, na mtoto wangu bahati mbaya alitoka nje bila kujua kama walikuwa wamevamia na katika kukimbia kujiokoa wakawa wamemvamia na kumchoma na bisibisi kifuani.

"Baadaye tulimkimbiza hospitalini, lakini alifariki dunia baada ya muda mfupi. Madaktari walipambana kuokoa maisha yake, lakini alikuwa amevuja damu nyingi," alisimulia.

Alisema mpaka jana jioni, mipango waliyokuwa nayo ni kusafirisha mwili kwenda mkoani Tanga kwa ajili ya maziko.

"Jana (juzi), Vingunguti kulichafuka, hilo kundi la hao panya road lilivamia na kuumiza watu na walikuwa wanasema wanalipa kisasi cha mwenzao ambaye anadaiwa naye aliuawa na wananchi," alisema Anna.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alisema watu saba wanashikiliwa na jeshi hilo kwa tuhuma za kumshambulia na kumsababishia kifo mwafunzi huyo pamoja na kujeruhi wengine wanane katika eneo la Vingunguti.

"Watuhumiwa hao wakiwa na wenzao katika kundi waliwashambulia wananchi mtaani maeneo ya Vingunguti kwa lengo la kulipiza kisasi wakati wakitoka kumzika mwenzao aliyefahamika kwa jina la Nurdin Bwiro.

"Bwiro aliuawa kwa kushambuliwa na wananchi alipokuwa na wenzake sita wakiwa na visu na vifaa mbalimbali vya kuvunjia, alipojaribu kuvunja nyumba moja usiku wa Julai 30 mwaka huu," alisema Kamanda Muliro.

# CHADEMA yaendelea kumsusia Msajili

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeendelea kumsusia Msajili wa Vyama vya Siasa kuhudhuria mikutano ya Baraza la Vyama vya Siasa baada ya jana kukacha kikao kilichofanyika jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, alisema hajui ni kwa nini hawajahudhuria na kwamba kati ya vyama 19 vyenye usajili wa kudumu ni CHADEMA pekee ambacho hakikuhudhuria mkutano huo.

"Baraza la vyama liliwaalika wote wamekuja ila hatujui kwa nini CHADEMA hawakuja, wanashida gani kwa sababu vyama vyote 18 vilikuwapo kasoro wao. Sisi tunawaasa wahudhurie vikao watu wanajadili maslahi ya nchi. Sijui wanataka wajadili na nani," alisema.

Alipoulizwa na Nipashe, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema ajenda za mkutano huo zilikuwa ushiriki wa viongozi wa dini, mavazi na vitendo vya walinzi wa vyama, lugha zinazotumiwa na viongozi kwenye mikutano ya vyama vya siasa.

"Kwa kuzitazama ajenda tunaona zinazungumzia masuala yaliyokwishawekewa utaratibu na haki zingine kwa mujibu wa Katiba, Sheria ya Vyama na sheria zingine za nchi. Hatukuona kama ni sahihi kwa sababu kabla ya mkutano msajili msaidizi alishaonyesha nia mbaya.

"Julai 22, mwaka huu, walituandikia barua wakitutaka tufute mkutano wa hadhara wakasambaza taarifa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, wakitaka tukajadili haya ambayo yameitwa leo kwa ajili ya baraza," alisema.

"CHADEMA tuliona ofisi ya msajili ina nia mbaya, mambo ya msingi hayana umuhimu. Kama kungekuwa na umuhimu wa baraza maalum kukutana kwa haraka agenda zingekuwa mbili kukwamua mchakato wa Katiba na marekebisho ya Katiba ya mpito kuwezesha uchaguzi wa serikali za mitaa mwakani na kama vyama tutafakari nini kuhusu mkataba wa uwekezaji bandarini wa kampuni ya DP World unaohitaji ushiriki wa vyama vyote,"aliongeza.

Kwa mujibu wa Mnyika, wakati nchi inataka kujadili hayo, wamebakiza miezi michache kuelekea ushaguzi wa serikali za mitaa lakini bado hakuna kinachowezesha uchaguzi huo kufanyika, kuna mambo ya kuitia dharura kuliko haya?

"Tumeona hakuna jambo lolote la dharura, yote yamewekewa utaratibu kwa mujibu wa Katiba, nasi tunaongozwa kwa Katiba," alisisitiza.

Mnyika alisema msajili na baraza la vyama waache kutumia vibaya fedha za walipakodi kulipa ukumbi, kodi, posho na mafuta kujadili mambo ambayo tayari yamewekewa utaratibu kwa mujibu wa Katiba.

"Ingepaswa tutumie muda huo kutukafari namna ya kupata mchakato wa Katiba, uchaguzi wa serikali za mitaa kwa kuwa na mabadiliko ya dharura, bunge litakwenda kwenye kikao Septemba mwaka huu tulitarajia hayo.

"CHADEMA tunawataka waite vikao kwa agenda za msingi na si kutumia fedha za walipakodi, basi hata wangetumia muda huo kutathimini utekelezaji wa ripoti ya kikosi kazi aliyoipokea rais," alisema Mnyika.

Aidha, alisema ni muhimu msajili akatafuta 'legitimacy' (uhalali) anakosa kwa sababu hasimamii vizuri Katiba,kanuni na sheria na akiendelea na vikao vya namna hii atazidi kupoteza.

# Raia wa Ukraine aunganishwa katika kesi uhujumu uchumi

**Na Kulwa Mzee**

RAIA wa Ukraine, Orga Kryshtopa, anayekabiliwa na mashtaka ya kusafirisha kobe 116 wenye thamani zaidi ya Sh, milioni 18 bila kibali, ameunganishwa katika kesi nyingine ya uhujumu uchumi yenye washtakiwa wanane, wakiwemo askari polisi wawili.

Orga alifutiwa kesi iliyokuwa ikimkabili jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Amir Msumi na kusomewa upya mbele ya hakimu huyo.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Orga, mfanyabiashara Joseph Moyo, Deogratius Lugeng'a, maofisa polisi Cosmas Ndomba na Kassim Abdallah, Hamza Juma, Nkanamuli Mgaza, Stephano Chedego na Mwaluko Mgomole.

Wakili wa Serikali, Pankrasia Protas, akiwasomea mashtaka yanayowakabili, alidai kuwa kati ya Januari Mosi na Julai 30, 2022 jijini Dar es Salaam, washtakiwa hao waliongoza genge la uhalifu kwa kununua, kuuza nyara za serikali ambazo ni kobe 116 wenye thamani ya Sh 18,935,840 mali ya serikali bila kibali.

Shtaka la pili, wanadaiwa kujihusisha na nyara za serikali bila kibali na shtaka la tatu inadaiwa katika tarehe hizo, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, washtakiwa walikutwa na nyara hizo bila kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Upande wa Jamhuri ulimaliza kuwasomea mashtaka na kudai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo kuomba shauri liahirishwe hadi tarehe nyingine ya kutajwa. Mahakama iliahirisha kesi hafi Agosti 9, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu Msumi aliwaeleza washtakiwa kuwa tarehe iliyopangwa shauri lao litasikilizwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Roda Ngimilanga aliyepangiwa.

Mshtakiwa Lugeng'a na Orga watawasilisha maombi yao ya dhamana kwa kuwa wako mahabusu. Washtakiwa wengine wako nje kwa dhamana.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura — Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji — ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni ya 20 (4) ya Kanuni za Mafuta Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Rejareja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)**

TAARIFA inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| **Jina la awali la kituo:** | **TFA Petrol Station - SEE Petroleum Co. Ltd** |
| **Nambari ya Leseni:** | **PRL-2020-354** |
| **Mahali Kituo kilipo:** | **Kiwanja Na. 14, Kitalu "II' Eneo la Barabara ya Uhuru Gangilonga, Wilaya ya Iringa, Mkoa wa Iringa** |
| **Jina linalopendekezwa:** | **Mega Planet Ltd** |
| **Mmiliki wa awali:** | **TFA Petrol Station - SEE Petroleum Co. Ltd** |
| **Mmiliki mpya:** | **Mega Planet Ltd** |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe ya tangazo hili.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA**

217533102



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura — Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji — ISO 9001:2015 Certified

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania na Kanuni ya 20 (4) ya Kanuni za Mafuta Biashara ya Jumla, Uhifadhi, Rejareja na Matumizi Binafsi), Gazeti la Serikali Toleo Na. 150 la 2022)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kubadili umiliki wa leseni na jina la kituo cha mafuta kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| **Jina la awali la kituo:** | **Petrolux Service Station Limited T/A Petrolux Bunda Service Station** |
| **Nambari ya Leseni:** | **PRL-2020-389** |
| **Mahali Kituo kilipo:** | **Kiwanja Na. 479, Kitalu "S" Eneo la Nyasura "D', Wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara** |
| **Jina linalopendekezwa:** | **GBP (T) Ltd T/A Bunda Service Station** |
| **Mmiliki wa awali:** | **Petrolux Service Station Limited Station** |
| **Mmiliki mpya:** | **GBP (T) Ltd** |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya mabadiliko ya umiliki na majina ya leseni tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne tokea tarehe ya tangazo hili.

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji – EWURA**

217533102

# Waziri aagiza mhandisi wa halmashauri achukuliwe hatua

**Na James Mwanamyoto**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, amemwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, Shadrack Mhagama, kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya Mhandisi Ujenzi wa Halmashauri hiyo, Daniel Kileo, kwa tuhuma za kushindwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi ya elimu.

Mhandisi huyo anatuhumiwa kushindwa kusimamia vizuri miradi hiyo ukiwamo wa ujenzi wa madarasa ya mradi wa BOOST, jambo ambalo ni kinyume cha maelekezo ya serikali yaliyotolewa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

Ndejembi alitoa maelekezo hayo jana mara baada ya kutoridhishwa na ujenzi wa madarasa akiwa katika ziara yake ya kikazi ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi inayojengwa na serikali kupitia miradi ya BOOST na SEQUIP.

Alisisitiza haiwezekani serikali itafute fedha za kujenga miundombinu ya elimu halafu zisitumike vizuri kutokana na mhandisi wa wilaya kushindwa kutafsiri ramani wakati yeye ndiye mtalaamu na mwenye jukumu hilo.


"Mkurugenzi mchukulie hatua za kinidhamu Mhandisi wa Ujenzi na mkaimishe mwingine kwa kuwa huyu ameshindwa kusimamia ujenzi wa madarasa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI itakuletea mhandisi mwingine atakayesimamia miradi ya ujenzi ya miundombinu ya elimu," aliagiza Ndejembi.

Baada ya ukaguzi wa miradi ya elimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Ndejembi alibaini miradi mingi katika halmashauri hiyo haijakamilika wakati katika wilaya zingine ikiwamo Manispaa ya Moshi imeshakamilika na changamoto kubwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ni kuwa na mhandisi ambaye ameonekana kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Ndejembi alisema amepewa taarifa kuwa katika Shule ya Sekondari Ashira bweni moja halijajengwa licha ya kuwa fedha zilishatolewa na serikali. Mhandishi ameshindwa kusimamia ujenzi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Kisare Makori, alimshukuru Ndejembi kwa kufanya ziara ya kukagua ujenzi wa miundombinu ya elimu na kuhimiza uwajibikaji katika wilaya yake ili miradi yote ikamilike kwa wakati na kuwanufaisha wananchi kama ilivyokusudiwa na serikali.

Makori pia alimwomba Ndejembi kumfikishia salamu za shukrani Rais Samia Suluhu Hassan kwa serikali kuipatia fedha nyingi wilaya yake kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za elimu, afya na miundombinu ya barabara.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto), akizungumza wakati wa semina iliyoambatana na uzinduzi wa ushirikiano baina ya benki hiyo na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), jijini Dar es Salaam jana, katika uendeshaji wa akaunti ya dhamana (Trust Account) kwa kampuni za bima nchini hatua inayolenga kuimarisha usimamizi wa sekta ya bima nchini ili kuendana na matakwa ya kisheria na udhibiti yaliyowekwa na **TIRA. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Kitila ataka uchumi utakaotengeneza matajiri

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Uwekezaji na Mipango, Prof. Kitila Mkumbo, amekabidhiwa ofisi na kuahidi kuwainua wajasiriamali wadogo na kutengeneza watanzania wengi matajiri.

Alikabidhiwa ofisi hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji katika Ofisi za Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

Kabla Rais Samia Suluhu Hassan kufanya mabadiliko hayo hivi karibuni, sekta ya uwekezaji ilikuwa imeunganishwa katika Wizara ya Viwanda na Biashara.

Waziri Kitila alisema anataka kuona halmashauri zote nchini zikiwa na mipango mbalimbali ya kuwainua wajasiriamali wadogo kiuchumi kwa kuwa ndiko kwenye idadi kubwa ya wananchi ambao wanafanya biashara ndogo.

"Kupitia halmashauri, huko ndiko tunaweza kuwainua watu wetu hawa wajasiriamali wadogo wakakuza uchumi wao. Lengo ni kuona tunakuwa na uchumi jumuishi unaondoa umaskini na unaotengeneza utajiri. Hili ndilo tunataka kuona linatokea katika nchi yetu," alisema

Prof. Kitila alisema mwelekeo wa nchi katika sekta ya uwekezaji una mambo makubwa ya kuzingatia ikiwamo kuendelea kuvutia wawekezaji wakubwa wapya kutoka nje ya nchi ili uchumi uendelee kukua na kuongeza ajira.

Prof. Kitila ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Maji na baadaye kuteuliwa na Rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli kuwa mbunge na Waziri wa Maji, alisema njia moja kubwa ya kukuza uchumi ni kuvutia uwekezaji mpya kwa kuweka mazingira mazuri.

"Kwa sasa mazingira ya uwekezaji ni bora kuwahi kutokea katika nchi hii na utulivu wa kisiasa ni mtaji mkubwa sana katika kuvutia uwekezaji. Lingine tunalojivunia ni utashi wa kisiasa wa Rais wetu katika kuvutia uwekezaji," alisema Prof. Kitila.

Aliongeza: "Kazi yangu kubwa itakuwa kuweka sheria nzuri na zile zinazokwaza biashara tutazifanyia marekebisho, tuone tunaendelea kuchochea wawekezaji wa nje na wa ndani tuwahamasishe, tuwape fursa tuwape mazingira mazuri waendelee kuwekeza ili tutengeneze matajiri," alisema.

Waziri huyo alisema miongoni mwa alivyokabidhiwa na Waziri Kijaji ni mchakato unaoendelea wa mapitio ya Sera ya Uwekezaji ya Mwaka 1996. Aliahidi kuuendeleza.

"Amenikabidhi pia Sheria ya Uwekezaji iliyopitishwa na Bunge mwaka 2022 na kanuni zake zimekamilika. Pia amenikabidhi bajeti ya 2023/24 kwa kipande cha uwekezaji na mpango wa maendeleo," alisema.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu, alisema tangu akabidhiwe wizara hiyo walifanikiwa kusajili miradi mipya 522 na wanatarajia miradi hiyo itasaidia kutengeneza ajira 72,000 kwa watanzania.

"Tunaona dhamira njema ya Rais wetu kuvutia wawekezaji. Safari nyingi za Rais nje ya nchi mliona tukitia saini makubaliano tangu Januari mpaka sasa ni makubaliano 50 ambayo tumeshaingia na nchi mbalimbali na kati ya hayo, 44 yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji, sita ndiyo bado tunafuatilia," alisema Waziri Kijaji.

## TIRA, NBC waingia ubia uendeshaji akaunti ya dhamana bima nchini

**Na Mary Geofrey**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imetangaza ushirikiano na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) katika uendeshaji wa akaunti ya dhamana (Trust Account) kwa kampuni za bima nchini .

Ni hatua inayotajwa kuimarisha usimamizi wa sekta ya bima nchini ili kuendana na matakwa ya kisheria na udhibiti yaliyowekwa na TIRA.

Ushirikiano huo ulitangazwa rasmi jana jijini Dar es Salaam wakati wa hafla fupi iliyokwenda sambamba na semina kwa wadau mbalimbali wa sekta ya bima nchini wakiwamo viongozi waandamizi kutokA TIRA, Benki ya NBC na wawakilishi wa kampuni za bima nchini wakiwamo wakurugenzi na maofisa wa fedha wa kampuni hizo.

Akizungumzia hatua hiyo, Kamishna wa Bima, Dk. Baghayo Saqware ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa TIRA, aliipongeza Benki ya NBC kwa kuanzisha akaunyo hiyo huku akibainisha kuwa hatua hiyo itasaidia sekta hiyo kuachana na utaratibu wa awali uliokuwa na upungufu kadhaa.

"Awali changamoto ilikuwa ni kwamba kampuni nyingi za bima zilikuwa ziNAtumia fedha za amana ya akiba katika matumizi mengine, pasipo kupata idhini ya TIRA, hivyo kupelekea kuingia katika changamoto ya ukwasi, na wakati mwingine kushindwa kulipa fidia kwa wateja kutokana na fedha kuwekezwa katika miradi mingine." alibainisha.

Alisema uamuzi wa kufungua akaunti ya dhamana ya bima katika benki za biashara ni suluhisho la changamoto hiyo, kwa kuwa sasa TIRA itaweza kusimamia moja kwa moja fedha hizo za amana za akiba, jambo ambalo si tu litaimarisha usimamizi, bali pia litaboresha maendeleo ya sekta ya bima nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi aliishukuru TIRA kwa kuipa fursa benki hiyo kushiriki katika uanzishwaji wa akaunti ya dhamana ya bima kwa kuwa utaleta uwazi na uwajibikaji katika sekta ya bima.

Sabi alipongeza uamuzi wa kuanzishwa kwa akaunti hiyo na kusisitiza kuwa ina mchango mkubwa katika kukuza uwazi zaidi na uwajibikaji katika sekta ya bima na itasaidia pia kujenga imani kwa wadau wa sekta hiyo.

Mkurugenzi wa Usimamizi wa TIRA, Abubakar Ndwata, alisema chimbuko la akaunti hiyo ya dhamana ya bima ni Kanuni za Bima za Mwaka 2009 zinazotaka kampuni za bima kuweka amana za usalama angalau asilimia 50 ya kiwango cha chini cha mtaji halisi wa kampuni husika ya bima.

## Taasisi kufanya utafiti tatizo sekta ya afya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, ameiagiza Taasisi ya Elimu ya Watumishi wa Afya Arusha (CEDHA), kujikita zaidi kufanya utafiti ambao utakaotoa majibu ya matatizo yanayoikabili sekta ya Afya.

Alisema endapo taasisi hiyo itajikita kufanya utafiti itasaidia kutoa majibu ya kuboresha sekta ya afya ikiwamo kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Mkuu huyo wa wilaya, alitoa agizo hilo juzi akiwa katika mahafali ya 36 miaka 40 tangu kuanzishwa kwa (CEDHA) na yaliyofanyika kwenye taasisi hiyo ya serikali.

Alisema nchi nyingi za Afrika hazina watafiti wa kutosha wa kutatua changamoto zake badala yake zinategemea watafiti kutoka nchi za nje kuwaletea majibu ya changamoto hizo jambo ambalo halina tija kwa maendeleo ya taifa lolote.

"Niombe sana vyuo hivi ambavyo vinashughulika na magonjwa ya binadamu kuzipatia ufumbuzi changamoto za afya zinazotuzunguka na tusipofanya hivyo tutajikuta tinatupwa nje na sekta yetu itakosa thamani na wananchi watakimbilia kwa waganga wa kienyeji ambao siyo wataalamu," alisema.

Pia, aliwataka wahitimu wa mafunzo hayo, kuhakikisha wanabeba dhana nzima ya taaluma ya afya kwa kuyaishi waliyofundishwa ili kwenda kuvisaidia vituo vya afya, zahanati na hospitali za hapa nchini kutoa huduma bora na yenye tija.

Katika hatua nyingine, alisema kuwa bajeti ya mwaka huu wa fedha serikali imefanya maboresho makubwa katika vituo vya afya na zahanati za Jiji la Arusha ikiwamo kuleta vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni sita.

Naye Mkuu wa (CEDHA), Dk. Johanes Lukumay, alisema taasisi hiyo iko chini ya serikali na imepewa majukumu makuu manne ikiwamo kutoa elimu kwa wakufunzi wa vyuo wa taaluma ya afya na kuwaendeleza kitaaluma watumishi wa sekta ya afya walioko kazini.

Pia, alisema majukumu mengine ni kufanya utafiti unaolenga kutatua changamoto zilizoko kwenye sekta ya afya na kutoa ushauri elekezi kuhusu masuala mbalimbali ya afya.

Alisema tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo, mwaka 1983 imekuwa taasisi ya kipekee na ya mfano inayotoa mafunzo ya stashahada ya ualimu wa vyuo vya taaluma za afya nchini.

Hata hivyo, alisema (CEDHA) imepiga hatua kubwa katika kufanya utafiti wa kuwaongezea ujuzi na maarifa wananchi kuhusu Ukimwi na afya ya uzazi.

# Madeleka azidi kusota mahabusu

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha imetupilia mbali ombi la kupatiwa dhamana Wakili wa Kujitegemea Peter Madeleka, hivyo anaendelea kusota mahabusu, akitakiwa kuripoti mahakamani Agosti 15 mwaka huu.

Akitoa uamuzi jana, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa mahakama hiyo, Fadhili Mbelwa, alisema mshtakiwa huyo anakabiliwa na makosa 10 ikiwamo la utakatishaji fedha ambalo halina dhamana, pia kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Juzi mahakamani huko, mawakili wa utetezi walioongozwa na Boniface Mwabukusi, waliiomba mahakama kumpatia mteja wao dhamana.

Kutokana na kuwapo mabishano ya kisheria ambayo yalitumia muda mwingi na kusababisha kuisha muda wa mahakama kufanya shughuli zake, Hakimu Mbelwa aliahirisha shauri hilo. Jana alitoa uamuzi huo. Ni uamuzi uliomfanya Wakili Madeleka aendelee kusota mahabusu hadi Agosti 15 mwaka huu, kesi itakapokuja kwa ajili ya kutajwa.

Nje ya mahakama hiyo, Wakili Mwabukusi alidai watakata rufani kupinga uamuzi huo katika mahakama za juu ili mteja wao apatiwe dhamana kwa kuwa wanaamini makosa anayodaiwa kutenda yanadhaminika.

"Kisheria hati ya mashtaka ikishafanyiwa marekebisho huwa inayotumika siyo ile tena ya awali. Sasa tunajiuliza hati ya awali ambayo ilikuwa na makosa 10, nani ameipeleka mahakamani ilhali ilishafanyiwa marekebisho ya kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu ambayo kosa lake lina dhamana?" alihoji Mwabukusi.

Madeleka alikamatwa akiwa kazini anatekeleza kazi zake Julai 17 mwaka huu, alipokuwa Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki, Mkoa wa Arusha.

Ni kesi ambayo upande wa utetezi una mawakili wanane wakiwamo Mwabukusi, Kennedy Chando, Denis Moses, Joseph Ole Shangay na Simon Mbwambo huku mawakili wa Jamhuri ni Upendo Shemkole, Tony Kilomo na Mahfudhu Mbagwa.



Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Afrika, Adam Mihayo (kulia), akikata utepe kuzindua huduma ya 'Bank of Africa Wakala' jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkuu wa Masoko na Mawasiliano, Nandi Mwiyombella (wa pili kushoto) na Mkuu wa Huduma za Kidigitali, Jesse Jackson (kushoto) na Meneja huduma wa Selcom, Galus Lutanya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nape: Vyombo vya habari vina nafasi kulinda usalama

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema vyombo vya habari vina nafasi kubwa ya kulinda usalama wa nchi na kutatua migogoro katika jamii.

Nape aliyasema hayo juzi alipofungua mafunzo ya kozi ya 15 kwa wahariri wa habari ya siku tano iliyoandaliwa na Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC).

Alisema vyombo vya habari vina nafasi kubwa katika kuimarisha usawa na kukuza umoja kwa kuwa vimefanya kazi nzuri ya kulijenga na kuimarisha taifa kwa miaka mingi.

"Ndiyo maana tumeendelea kubaki salama. Mnazijua nchi ambazo zimepitia misukosuko mikubwa kwa sababu wa wanahabari wake kutowajibika. Tanzania wanahabari wake wako tofauti, wanafanya kazi nzuri. Siyo vibaya baada ya kufanya kazi nzuri kupitia upya na kutafakari kuona kama tunaweza kufanya vizuri zaidi,"alisema Nape.

Alisema taifa ni mchanganyiko wa jamii ambayo ina tamaduni mbalimbali, kukiwa na makabila zaidi ya 120. Wanashikamana na kuendelea kuwa taifa moja.

"Tunayo mataifa ambayo yana makabila machache na tamaduni chache, lakini wameshindwa kukaa pamoja. Ni wajibu wetu kuendelea kuliona taifa letu likiwa wamoja na tujivunie utaifa wetu," alisema Nape

Alisema mafunzo hayo yatawasaidia kupata mkakati wa kuliona taifa linaendelea kuwa kitu kimoja na kuheshimu misingi iliyopo.

Kwa mujibu wa Nape, taifa limejengwa katika misingi imara ya sheria, katiba na taratibu ambazo zinaifanya taifa liende vizuri, hivyo ni wajibu wao kuhakikisha taifa linaendelea kubaki salama, kusiwapo ukiukwaji wa sheria na matumizi mabaya ya rasilimali.

"Umuhimu wa kuendelea kuijenga haki katika jamii yetu, kuhakikisha hakuna ukiukwaji wa sheria, matendo ya kifisadi ya kuharibu na matumizi mabaya ya rasilimali za nchi yetu,"alisema Nape.

Alisema waandishi wa habari wana uwezo wa kupinga chuki na uchochezi katika jamii kwa kuchapisha nakala za kusisitiza umuhimu wa kuheshimu jamii, siasa, dini na utamaduni.

Nape alisema waandishi wa habari wanaweza kuwa sauti za busara na kusaidia kuzuia migogoro na kuimarisha amani katika jamii na taifa kwa ujumla.

Mkuu wa Chuo cha NDC, Meja Jenerali Ibrahim Mhona, alisema mafunzo hayo yataleta matokeo chanya na kulifanya taifa kuendelea kuwa salama.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tahadhari iliyotolewa TMA isipuuzwe

**HIVI** karibuni Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini (TMA), ilitoa tahadhari ya kuwapo kwa mvua ya El-Nino huku ikitaja mikoa tisa kukumbwa na mvua hiyo.

Madhara yanayosababishwa na El-Nino ni makubwa kwa sababu mvua hunyesha kubwa na inayoambatana na upepo mkali.

Matokeo ya mvua hiyo ni kuharibika kwa miundombinu ya barabara, nyumba kubomoka, mazao kusombwa na vitu vingi kuharibika.

Tahadhari ya TMA ni kuwafanya watu wajiandae kuboresha nyumba wanazoishi ili hata mvua hiyo inapokuja iwakute katika nyumba salama na kuepusha athari.

Miundombinu ya barabara pia inatakiwa kuboreshwa, mifereji inayopitisha maji barabarani izibuliwe ili hata kunapotokea mafuriko maji ya mvua yapite kwa urahisi kwenye mifereji hiyo.

Watu wanaotupa taka kwenye mifereji wanatakiwa kuacha tabia hiyo kwa sababu mifereji itakapoziba, waathirika wakubwa ni wao wenyewe na kilio hupelekwa kwa serikali wakati chanzo cha kuziba mifereji hiyo ni wao wenyewe.

Kuna watu bila aibu huchukua viroba vya taka kwenye nyumba zao na kwenda kuvitupa kwenye mifereji.

Hata wanaofanya biashara kando ya barabara wamegeuza mifereji hiyo kama madampo ya kutupa taka zao wanapomaliza shughuli zao.

Wananchi lazima wajifunze ustaarabu wa kuhifadhi mazingira na kuyaweka katika hali ya usafi ili kuepusha athari zinazoweza kudhibitiwa.

TMA imeendelea kutoa tahadhari ya kuwapo kwa upepo mkali na mawimbi makubwa katika maeneo ya ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi, maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa.

Katika taarifa yake iliyotolewa juzi imesema kunatarajiwa kuwapo kwa upepo unaofikia kilometa 40 kwa saa na mawimbi makubwa yanayofika mita mbili katika maeneo hayo ya mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Lindi, Mtwara na Zanzibar, Mwanza, Simiyu, Kagera, Geita, Mara, Kigoma, Katavi na Rukwa.

Mtaalam wa hali ya hewa kutoka TMA amewataka wananchi katika maeneo hayo kuchukua tahadhari kukabiliana na hali hiyo.

Mamlaka hiyo imefafanua kuwa kuanzia Jumatano (leo) mpaka Ijumaa na kwa mujibu wa mifumo ya hali ya hewa, uwezekano wa kutokea upepo huo ni mkubwa.

Athari zake ni pamoja na kukwama kwa shughuli za uvuvi na usafirishaji na shughuli nyingine za kiuchumi. Kwa mujibu wa Mamlaka hiyo.


Wananchi wametakiwa kutopuuza taarifa za tahadhari zinazotolewa na mamlaka hiyo na wanapaswa kuchukua hatua kuepuka madhara na athari zinazoweza kutokea.

TMA inaendelea kufuatilia mifumo ya hali ya hewa na inaendelea kutoa taarifa kwa wananchi, imeomba sana wananchi kufuatilia taarifa za hali ya hewa wanazozitoa kila wakati.

Ufuatiliaji wa hali ya hewa katika vyombo vya habari unasaidia kujua hali kwa siku hiyo ikoje. Kwa nchi wenzetu mtu hawezi kutoka nyumbani kwake bila kuangalia hali ya hewa ili aweze kujiandaa, kama kuna mvua atatayarisha vifaa vya kujikinga na kama siku hiyo kutakuwa na baridi, basi atajiandaa kwa nguo nzito ili kujikinga.

Ufuatiliaji wa hali ya hewa unasaidia sana mtu kujiandaa na kujiepusha na madhara yanayoweza kuyapata.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Unashangaza ukatili kuwatosa mapacha

**NGUVU** kubwa za wadau wa kupambana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, zimekuwa zikielekezwa katika kukabili vipigo, kunyanyasaja wajane, ulawiti, ubakaji , mimba na ndoa za utotoni, utumikishwaji majumbani hasa kwa watoto.

Hata hivyo, lipo eneo lililoshamiri vitendo hivyo, ambalo inaelezwa kuwa halijapewa uzito kwa ajili ya kukabiliana nalo, ambalo linahusisha wanaume kutekelezwa wanawake zao wanapojifungua mapacha.

Sababu kubwa ambayo inatajwa katika ukatili huo, ni baadhi yao katika mila zao kuamini kuwa ni mkosi mwanamke kujifungua watoto wawili, watatu au wanne kwa mpigo.

Katika mazingira hayo, baadhi ya wanawake wenye watoto hao hasa wale ambao hawana fedha wanajikuta katika wakati mgumu kukabiliana na mazingira hayo ya kulea mapacha bila msaada kutoka kwa wazazi wenza.

Tatizo hili nalo linapaswa kuchukuliwa kama ukatili wa kijinsia, ili wanaotekeleza wake zao au wapenzi wao, kwa sababu ya kuzaa mapacha washurutishwe kulea watoto wao badala ya kuwakimbia.

Mtindo huo wa baadhi ya wanaume kufanya ukatili huo, umeibuliwa na taasisi isiyo ya kiserikali Eden Twins Foundation yenye maskani yake mkoani Pwani, ambayo mwenyekiti wake anatamani utambuliwe kama ukatili.

Ninaungana na mwenyekiti huyo Diana Mbena, kwamba huo unapaswa kuwa ukatili wa kijinsia, mbaya zaidi wapo wanaowapa ujauzito watu wenye ulemavu na kuwatelekeza, hali inayowaongezea mzigo.

Kwa mfano, kuna mlemavu kipofu ambaye anaishi Mbagala Charambe Dar es Salaam, aliyejifungua mapacha na kukimbiwa na mzazi mwenzake, kwa maelezo kwamba kwao hawazai mapacha.

Ninaamini kwamba kwa ulemavu alionao, mzazi mwenzake angekuwa msaada mkubwa katika kulea watoto, lakini matokeo yake akakimbia huku akitoa sababu ambazo hazina mantiki.

Ni kweli kwamba si wote wanaojifungua watoto mapacha hawana uwezo wa kulea, lakini baadhi yao hawana, badala yake wamekuwa wakitegemea msaada kutoka kwenye jamii, huku waliowazalisha wakiendelea na maisha kwingine.

Inawezekana serikali ikafuatilia zaidi kubaini ukubwa kwa tatizo hilo, kwani kwa mujibu wa mwenyekiti wa Taasisi ya Eden, ni kwamba alishafuatilia katika mikoa ya Pwani na Dar es Salaam na kubaini kuwa familia nyingi zenye watoto mapacha ni zile zilizo na uwezo mdogo kiuchumi.

Kwa mazingira kama hayo, ni wazi familia hizo zinaweza kushindwa kuwahudumia watoto hao kuanzia matibabu, lishe na hata mavazi, hivyo kundi hilo lingetazamwa kwa jicho la ziada.

Huwa ni kawaida kumpongeza aliyejifungua mapacha, lakini pia ni vyema kuangalia mazingira aliyomo na vikwazo anavyokutana navyo anapohudumia watoto wake, ili aweze kusaidiwa kama atakuwa na hali ngumu kiuchumi.

Njia nyingine inayoweza kuwasaidia, ni kuwatambua na kuangalia uwezekano wa kuwapa bima, kwani kutegemea kuwa watoto wadogo wanatibiwa bure, wengi wao wanaweza kukosa matibabu wanapopelekwa hospitali kwa kuambiwa kwamba hakuna dawa wakanunue duka la jirani na hospitali.

Wakiwa na bima hata wakienda hospitali yoyote wanaweza kupata matibabu. Pia ikumbukwe kuwa suala la kuzaa mapacha, Mungu anaweza kumpa mwenye uwezo kiuchumi na asiye na uwezo huo.

Lakini pamoja na hayo, ni vyema kutambua kuwa mume kumkimbia mkewe aliyejifungua mapacha, ni ukatili wa kijinsia ambao unapaswa kupigwa vita na wadau wote wanaotetea haki za wanawake na watoto.

Kwa mtazamo wangu ni kwamba, mambo ya mila kwamba ni mkosi kuzaa mapacha au mengine yanayofanana na hayo,, hayapaswi kuwa kichaka na kujificha kwa wale wanaotelekeza familia zao zenye watoto wa aina hiyo.

Ninaamini ikiendeshwa vita dhidi ya watu wenye tabia na mtindo wa kukimbia wanawake waliojifungua watoto mapacha, tatizo hili linaweza kuisha na hivyo kufanya familia kuwa na amani na furaha kwa kupata huduma zote muhimu.

# Makamu wa Rais atoa angalizo ukarabati wa mashine ya MRI

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amezindua huduma ya kipimo cha mashine ya MRI katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya na kuagiza uongozi wa hospitali hiyo kutumia vizuri ili itumike kwa muda mrefu.

Dk. Mpango alizindua mashine hiyo jana ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kukagua miradi ya maendeleo mkoani Mbeya ambapo mashine hiyo imefungwa katika Jengo la Mionzi la hospitali hiyo.

Aliagiza muda uliopangwa kitaalamu wa ajili ya kufanyia ukarabati uzingatiwe ili kuhakikisha mashine hiyo inafanya kazi kwa muda mrefu.

"Mashine hii imegharimu Sh. bilioni tatu, ni fedha nyingi. Kwa hiyo, ninaomba watumishi wote wa hospitali hii kuhakikisha mnaitunza ili itusaidie kwa muda mrefu, ifanyiwe ukarabati kwa kuzingatia muda ambao umeainishwa," aliagiza Dk. Mpango.

Katika hatua nyingine, Makamu wa Rais aliagiza Shirika la Viwango (TBS) na Wizara ya Viwanda na Biashara kwenda kukagua magari maalum ya kubeba wagonjwa yaliyobuniwa na wataalamu wa hospitali hiyo ya kanda.

Magari hayo yamebuniwa na wataalamu wa hospitali hiyo ili yatumike kubeba wagonjwa ndani ya hospitali na yatatumika kama mbadala wa machela na vitanda vyenye magurudumu.

Alisema magari hayo yakibainika kuwa yana ubora yanatakiwa yapewe ithibati ili yatumike katika hospitali zote nchini kwa ajili ya kubeba wagonjwa.

Pia aliagiza wataalamu wa hospitali hiyo waliobuni magari hayo wawezeshwe kuzalisha mengi zaidi na waongezwe mishahara ili wafanye kazi hiyo kwa moyo zaidi.

Vilevile, aliagiza Wizara ya Afya kwa kushirikiana na viongozi wa hospitali hiyo kuharakisha mchakato wa kuifanya hospitali hiyo kuwa taasisi na kuundwa bodi ya wakurugenzi ili kuboresha zaidi huduma kwa wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na nchi jirani za ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema madaktari wa hospitali hiyo wana ubunifu mkubwa ambao umesababisha huduma kuendelea kuwa bora katika ukanda huo wa Nyanda za Juu Kusini.

Alisema mbali na ubunifu wa magari ya kubeba wagonjwa, wataalamu wa hospitali hiyo pia wamebuni mifumo maalum ya kubaini mwanamke aliyefanyiwa upasuaji kama anavuja damu. Unatoa taarifa kwa madaktari.

Vilevile, alisema wamebuni mfumo maalum wa kurekebisha kiwango cha joto katika chumba cha kutoa huduma kwa watoto njiti ambao joto likizidi unazima mashine ya joto.

Pia alisema, kutokana na umahiri wa utoaji wa huduma wa hospitali hiyo, wataalamu wake wamealikwa kuwajengea uwezo wataalamu wa nchi mbalimbali za Afrika zikiwamo Ethiopia na Afrika Kusini.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Dk. Godlove Mbwanji, alisema kuwa kabla ya kuanza kutumika mashine hiyo ya MRI, wananchi waliokuwa wanahitaji kipimo hicho walikuwa wanalazimika kusafiri umbali mrefu kwenda kuitafuta.

Alisema wananchi wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini walikuwa wanasafiri kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) au Dodoma katika Hospitali ya Benjamin Mkapa.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliishukuru serikali kwa uboreshaji wa huduma za afya katika Mkoa wa Mbeya. Mbali na hospitali hiyo ya rufani ya kanda, serikali pia imejenga vituo vya afya na zahanati.



Makamu wa Rais wa AngloGold Ashanti- GGML anayeshughulikia miradi endelevu kwa Ghana na Tanzania, Simon Shayo (kushoto), akichangia mjadala wa nishati kupitia Jukwaa la fikra la Mwananchi, jijini Dar es Salaam juzi. Wengine ni washiriki wa mjadala huo ulioenda sambamba na uzinduzi wa mpango mkakati wa miaka 10 wa Tanesco. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Tupo tayari kuwapa ushirikiano TANESCO'

**Na Halfani Chusi**

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imesema ipo tayari kushirikiana kikamilifu na Shirika la Umeme nchini (TANESCO) kwa kutumia umeme wa Gridi ya Taifa baada ya ujenzi wa kituo cha kupoza umeme na mradi wa kupeleka umeme katika migodi ya kampuni hiyo kukamilika.

Pia imeipongeza TANESCO na Wizara ya Nishati kwa kuja na mpango mkakati wa miaka 10 ambao utaliwezesha shirika hilo kuanzisha vyanzo vipya vya nishati endelevu kwa kuwa ni jambo litakalolisaidia taifa kutimiza lengo namba saba la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) linalozungumzia matumizi ya nishati inayofikika, ya gharama nafuu, endelevu na ya kisasa kwa wananchi wake.

Makamu Rais wa AngloGold Ashanti - GGML anayeshughulikia miradi endelevu kwa upande wa Ghana na Tanzania, Simon Shayo aliyasema hayo juzi alipochangia mjadala wa nishati kupitia Jukwaa la Fikra la Mwananchi.

Shayo alisema mpango huo mkakati wa miaka 10, utaifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza kusini mwa nchi za Jangwa la Sahara kutimiza lengo hilo la maendeleo endelevu (SDG).

"Ni hatua kubwa kwa TANESCO kutafsiri kwenye mkakati wake lile lengo namba saba," alisema Shayo.

Alisema licha ya kwamba kampuni nyingi za madini tangu miaka ya 2000 hutumia umeme wanaouzalisha wenyewe, sasa serikali imekuwa na jitihada za makusudi kufungamanisha sekta ya nishati na sekta kubwa za uzalishaji kwa kuzalisha umeme unaotosheleza mahitaji ya wawekezaji wakubwa.

"Sisi kwa sekta ya madini tunaona hii kama ni baraka kubwa kwa sababu huwezi kuendesha migodi mikubwa kama ya kwetu (GGML) kwa kutumia jenereta," alisema.

Alitoa mfano kuwa GGML hutumia Megawati 29 ambazo huzalisha kwa mafuta lakini sasa wanatamani kuona mradi wa kupeleka umeme wa TANESCO katika mgodi wa kampuni hiyo ukikamilika ili kupunguza gharama za uendeshaji.

"Tukijiunga tu na TANESCO kwenye Gridi ya Taifa na kutoka kwenye umeme tunaouzalisha wenyewe, tutapunguza gharama za umeme kwa asilimia 50, tutaokoa dola za Marekani milioni 19 kila mwaka. Pia tutapunguza hewa ukaa kilotons 81 kufikia 2030," alisema.

Shayo alisema kwa kuwa nchi ipo katika mipango ya kuwekeza pakubwa katika sekta ya madini kwa kuanzisha migodi ya uzalishaji wa madini mengine sehemu mbalimbali nchini, ni dhahiri kuwa TANESCO itafanikiwa kuongeza mapato makubwa kutokana na mchango wa migodi hiyo katika matumizi ya umeme.

Alisema shirika linajenga laini ya kilovolt 220 kutoka Bulyanhulu hadi Geita kisha laini ya kilomita sita yenye kilovolt 33 kuelekea katika mgodi wa GGML wakati kampuni hiyo inajenga kituo cha kupoza umeme kwenda kilovolt 11 kwa gharama ya dola za Marekani milioni 24.4.

Awali akizindua mpango huo mkakati wa TANESCO, Waziri wa Nishati, Januari Makamba, aliwataka wananchi wawe na subira wakati shirika hilo linafanya mageuzi ya utendaji kazi wake.

Alisema serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuipa mtaji TANESCO ili itekeleze mipango yake kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa wananchi na Afrika kwa ujumla.

Mkurugenzi wa TANESCO, Maharage Chande, alisema shirika hilo linakusudia kuendelea na mipango yake ya kuboresha huduma kwa wateja wake, kupitia miradi mbalimbali ikiwamo wa kufua umeme katika Bwawa la Julius Nyerere, ambao unatarajia kuanza kuzalisha umeme Juni mwakani.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001:2015 Certified

## KUMB: PPR/2023 - 08/01

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 2 AGOSTI 2023

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini zitakazotumika kuanzia Jumatano, tarehe **2 Agosti 2023 saa 6:01 usiku.** Kwa mwezi Agosti 2023, bei za rejareja za mafuta katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ni kama ifuatavyo:

| Mkoa | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| | TZS/Lita | | |
| Dar es Salaam | 3,199 | 2,935 | 2,668 |
| Tanga | 3,245 | 2,981 | 2,740 |
| Mtwara | 3,271 | 3,008 | 2,714 |

Mabadiliko ya bei za mafuta kwa mwezi Agosti 2023 yanatokana na changamoto za **upatikanaji wa Dola za Marekani, mabadiliko ya sera za kikodi, kushuka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani, ongezeko la gharama za mafuta katika soko la dunia na gharama za uagizaji wa mafuta.** Bei za mafuta katika miji, wilaya na mikoa ni kama zinavyooneshwa katika **Jedwali Na. 1** na bei za mafuta kwa wafanyabiashara wa jumla ni kama zinavyooneshwa katika **Jedwali Na. 2.**

Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika Jedwali Na. 1. Aidha, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika Jedwali Na. 2. **Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.**

EWURA inapenda kuwakumbusha wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na jamii kuzingatia yafuatayo: -

a) bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.

b) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015,** kifungu namba 166, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta.

c) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani isipokuwa bei hizo zisizidi **bei kikomo (Price cap) au kuwa chini ya bei iliyoruhusiwa (Floor Price) kama zilivyokokotolewa kwa mujibu wa Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2023 zilizotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 421 la tarehe 23 Juni 2023.**

d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana yakionesha bei za mafuta, punguzo, vivutio vya kibiashara vinavyotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**

e) Wauzaji wa bidhaa za mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa stakabadhi za mauzo kutoka kwenye Electronic Fiscal Pump Printers (EFPP) na wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora unaotakiwa. Stakabadhi hizo pia zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya bidhaa za mafuta ya petroli.

**JEDWALI 1:** BEI KIKOMO ZA REJAREJA KWA SHILINGI/LITA

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
| **Dar es Salaam** | **3,199** | **2,935** | **2,668** |
| **Arusha** | **3,283** | **3,038** | **2,752** |
| Arumeru (Usa River) | 3,283 | 3,038 | 2,752 |
| Karatu | 3,301 | 3,056 | 2,770 |
| Longido | 3,294 | 3,049 | 2,763 |
| Monduli | 3,289 | 3,043 | 2,757 |
| Monduli-Makuyuni | 3,294 | 3,048 | 2,762 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 3,375 | 3,123 | 2,843 |
| **Coast (Kibaha)** | **3,204** | **2,940** | **2,672** |
| Bagamoyo | 3,210 | 2,946 | 2,679 |
| Bagamoyo (Miono) | 3,241 | 2,977 | 2,709 |
| Bagamoyo (Mbwewe) | 3,222 | 2,958 | 2,690 |
| Chalinze Junction | 3,213 | 2,949 | 2,682 |
| Chalinze Township (Msata) | 3,217 | 2,953 | 2,686 |
| Kibiti | 3,219 | 2,956 | 2,688 |
| Kisarawe | 3,206 | 2,942 | 2,675 |
| Mkuranga | 3,209 | 2,945 | 2,677 |
| Rufiji | 3,227 | 2,963 | 2,695 |
| **Dodoma** | **3,258** | **2,994** | **2,726** |
| Bahi | 3,265 | 3,001 | 2,734 |
| Chamwino | 3,253 | 2,989 | 2,722 |
| Chemba | 3,284 | 3,020 | 2,753 |
| Kondoa | 3,291 | 3,027 | 2,759 |
| Kongwa | 3,255 | 2,991 | 2,724 |
| Mpwapwa | 3,259 | 2,995 | 2,728 |
| Mpwapwa (Chipogoro) | 3,271 | 3,007 | 2,740 |
| Mtera (Makatopora) | 3,277 | 3,013 | 2,745 |
| Mvumi | 3,264 | 3,000 | 2,733 |
| **Geita** | **3,364** | **3,101** | **2,833** |
| Bukombe | 3,353 | 3,089 | 2,822 |
| Chato | 3,386 | 3,122 | 2,854 |
| Mbogwe | 3,403 | 3,139 | 2,871 |
| Nyang'hwale | 3,380 | 3,116 | 2,848 |
| **Iringa** | **3,263** | **2,999** | **2,732** |
| Ismani | 3,268 | 3,004 | 2,737 |
| Kilolo | 3,268 | 3,004 | 2,736 |
| Mufindi (Mafinga) | 3,273 | 3,009 | 2,742 |
| Mufindi (Igowole) | 3,282 | 3,018 | 2,750 |

# TANGAZO

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
| **Kagera (Bukoba)** | **3,415** | **3,151** | **2,883** |
| Biharamulo | 3,389 | 3,125 | 2,858 |
| Karagwe (Kayanga) | 3,431 | 3,167 | 2,900 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 3,437 | 3,173 | 2,905 |
| Muleba | 3,415 | 3,151 | 2,883 |
| Ngara | 3,402 | 3,138 | 2,871 |
| Misenyi | 3,423 | 3,159 | 2,892 |
| **Katavi (Mpanda)** | **3,357** | **3,093** | **2,825** |
| Mlele (Inyonga) | 3,339 | 3,075 | 2,807 |
| Mpimbwe (Majimoto) | 3,376 | 3,112 | 2,845 |
| Tanganyika (Ikola) | 3,375 | 3,111 | 2,843 |
| Kigoma | 3,361 | 3,097 | 2,830 |
| Uvinza (Lugufu) | 3,352 | 3,088 | 2,820 |
| Muyobozi Village (Uvinza) | 3,360 | 3,096 | 2,829 |
| Ilagala Village (Uvinza) | 3,362 | 3,098 | 2,831 |
| Buhigwe | 3,360 | 3,096 | 2,829 |
| Kakonko | 3,362 | 3,098 | 2,831 |
| Kasulu | 3,371 | 3,107 | 2,839 |
| Kibondo | 3,368 | 3,104 | 2,837 |
| **Kilimanjaro (Moshi)** | **3,273** | **3,028** | **2,741** |
| Hai (Bomang'ombe) | 3,276 | 3,031 | 2,745 |
| Mwanga | 3,266 | 3,021 | 2,735 |
| Rombo (Mkuu) | 3,294 | 3,044 | 2,762 |
| Same | 3,259 | 3,014 | 2,728 |
| Siha (Sanya Juu) | 3,279 | 3,034 | 2,748 |
| **Lindi** | **3,258** | **2,994** | **2,727** |
| Lindi-Mtama | 3,276 | 3,012 | 2,745 |
| Kilwa Masoko | 3,233 | 2,969 | 2,702 |
| Liwale | 3,279 | 3,015 | 2,748 |
| Nachingwea | 3,287 | 3,023 | 2,756 |
| Ruangwa | 3,289 | 3,025 | 2,757 |
| **Manyara (Babati)** | **3,321** | **3,072** | **2,790** |
| Hanang (Katesh) | 3,332 | 3,083 | 2,801 |
| Kiteto (Kibaya) | 3,333 | 3,087 | 2,801 |
| Mbulu | 3,334 | 3,085 | 2,803 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 3,354 | 3,104 | 2,822 |
| **Mara (Musoma)** | **3,365** | **3,101** | **2,833** |
| Musoma Vijijini (Busekela) | 3,378 | 3,114 | 2,846 |
| Rorya (Ingirijuu) | 3,372 | 3,108 | 2,840 |
| Rorya (Shirati) | 3,380 | 3,116 | 2,848 |
| Bunda | 3,356 | 3,092 | 2,825 |
| Bunda (Kisorya) | 3,369 | 3,105 | 2,837 |
| Butiama | 3,362 | 3,098 | 2,831 |
| Serengeti (Mugumu) | 3,373 | 3,109 | 2,842 |
| Tarime | 3,373 | 3,109 | 2,842 |
| Tarime (Kewanja/Nyamongo) | 3,379 | 3,115 | 2,848 |
| **Mbeya** | **3,306** | **3,042** | **2,775** |
| Chunya | 3,316 | 3,052 | 2,784 |
| Chunya (Makongolosi) | 3,321 | 3,057 | 2,790 |
| Chunya (Lupa Tingatinga) | 3,323 | 3,059 | 2,792 |
| Kyela | 3,322 | 3,058 | 2,791 |
| Mbarali (Rujewa) | 3,290 | 3,026 | 2,759 |
| Rujewa (Madibira) | 3,304 | 3,040 | 2,772 |
| Rujewa (Kapunga) | 3,300 | 3,036 | 2,769 |
| Rungwe (Tukuyu) | 3,315 | 3,051 | 2,784 |
| Busokelo (Iwangwa) | 3,318 | 3,054 | 2,787 |
| **Morogoro** | **3,224** | **2,960** | **2,693** |
| Mikumi | 3,240 | 2,976 | 2,708 |
| Kilombero (Ifakara) | 3,262 | 2,998 | 2,731 |
| Kilombero (Mlimba) | 3,284 | 3,020 | 2,753 |
| Kilombero (Mngeta) | 3,273 | 3,010 | 2,742 |
| Ulanga (Mahenge) | 3,273 | 3,009 | 2,741 |
| Malinyi | 3,283 | 3,019 | 2,751 |
| Kilosa | 3,242 | 2,979 | 2,711 |
| Gairo | 3,242 | 2,979 | 2,711 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 3,234 | 2,971 | 2,703 |
| Mvomero (Sanga Sanga) | 3,224 | 2,960 | 2,693 |
| Turian | 3,249 | 2,985 | 2,718 |
| **Mtwara** | **3,271** | **3,008** | **2,740** |
| Nanyumbu (Mangaka) | 3,320 | 3,056 | 2,789 |
| Masasi | 3,297 | 3,033 | 2,766 |
| Newala | 3,304 | 3,040 | 2,772 |
| Tandahimba | 3,297 | 3,033 | 2,765 |
| Nanyamba | 3,297 | 3,033 | 2,765 |
| **Mwanza** | **3,349** | **3,085** | **2,818** |
| Kwimba | 3,367 | 3,103 | 2,836 |
| Magu | 3,357 | 3,093 | 2,826 |
| Misungwi | 3,344 | 3,080 | 2,812 |
| Misungwi (Mbarika) | 3,354 | 3,090 | 2,822 |


| Mji | Bei Kikomo | | |
|---|---|---|---|
| | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
| Sengerema | 3,382 | 3,118 | 2,850 |
| Ukerewe | 3,409 | 3,145 | 2,877 |
| **Njombe** | **3,292** | **3,028** | **2,760** |
| Njombe (Kidegembye) | 3,312 | 3,048 | 2,781 |
| Ludewa | 3,329 | 3,065 | 2,798 |
| Makambako | 3,284 | 3,020 | 2,752 |
| Makete | 3,322 | 3,058 | 2,791 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 3,289 | 3,025 | 2,758 |
| **Rukwa (Sumbawanga)** | **3,372** | **3,108** | **2,841** |
| Sumbawanga Rural (Mtowisa) | 3,372 | 3,108 | 2,841 |
| Kalambo (Matai) | 3,379 | 3,115 | 2,848 |
| Nkasi (Namanyele) | 3,386 | 3,122 | 2,854 |
| Nkasi (Kirando) | 3,395 | 3,131 | 2,864 |
| **Ruvuma (Songea)** | **3,322** | **3,059** | **2,791** |
| Mbinga | 3,335 | 3,071 | 2,804 |
| Namtumbo | 3,328 | 3,064 | 2,796 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 3,345 | 3,081 | 2,814 |
| Tunduru | 3,302 | 3,038 | 2,771 |
| **Shinyanga** | **3,328** | **3,064** | **2,797** |
| Kahama | 3,332 | 3,068 | 2,801 |
| Kishapu | 3,336 | 3,072 | 2,805 |
| Ushetu (Nyamilangano) | 3,344 | 3,080 | 2,813 |
| Ushetu (Kangeme Village) | 3,350 | 3,086 | 2,819 |
| Salawe | 3,342 | 3,078 | 2,810 |
| **Simiyu (Bariadi)** | **3,346** | **3,082** | **2,815** |
| Busega (Nyashimo) | 3,358 | 3,094 | 2,827 |
| Itilima (Lagangabilili) | 3,346 | 3,082 | 2,815 |
| Maswa | 3,340 | 3,076 | 2,808 |
| Meatu (Mwanhuzi) | 3,351 | 3,087 | 2,819 |
| **Singida** | **3,290** | **3,026** | **2,758** |
| Iramba | 3,302 | 3,038 | 2,771 |
| Manyoni | 3,274 | 3,011 | 2,743 |
| Itigi (Mitundu) | 3,290 | 3,026 | 2,759 |
| Ikungi | 3,285 | 3,021 | 2,754 |
| Mkalama (Nduguti) | 3,314 | 3,050 | 2,783 |
| **Songwe (Vwawa)** | **3,315** | **3,051** | **2,784** |
| Songwe (Mkwajuni) | 3,322 | 3,058 | 2,791 |
| Ileje | 3,319 | 3,055 | 2,788 |
| Momba (Chitete) | 3,325 | 3,061 | 2,793 |
| Tunduma | 3,320 | 3,056 | 2,788 |
| **Tabora** | **3,307** | **3,043** | **2,776** |
| Igunga | 3,307 | 3,043 | 2,776 |
| Kaliua | 3,320 | 3,056 | 2,789 |
| Ulyankulu | 3,318 | 3,054 | 2,786 |
| Nzega | 3,318 | 3,054 | 2,786 |
| Sikonge | 3,316 | 3,052 | 2,785 |
| Urambo | 3,317 | 3,053 | 2,786 |
| Uyui | 3,314 | 3,050 | 2,782 |
| Mpyagula | 3,339 | 3,075 | 2,808 |
| **Tanga** | **3,245** | **2,981** | **2,714** |
| Handeni | 3,225 | 3,002 | 2,693 |
| Kilindi | 3,259 | 3,017 | 2,728 |
| Korogwe | 3,238 | 2,994 | 2,707 |
| Lushoto | 3,248 | 3,003 | 2,717 |
| Mkinga (Maramba) | 3,259 | 2,988 | 2,728 |
| Muheza | 3,245 | 2,986 | 2,714 |
| Pangani | 3,252 | 2,988 | 2,720 |

**JEDWALI 2:** BEI KIKOMO ZA JUMLA (SHILINGI/LITA)

| Bandari | Petroli | Dizeli | Mafuta ya Taa |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 3,067.10 | 2,803.56 | 2,537.61 |
| Tanga | 2,985.40 | 2,849.80 | - |
| Mtwara | 2,662.38 | 2,867.94 | - |

Dkt. James A. Mwainyekule

**MKURUGENZI MKUU- EWURA**



# Wananchi waikataa zahanati kisa vioo

**Na Shaban Njia,** USHETU.

WANANCHI wa Kijiji cha Nyamtengela, Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameikataa zahanati waliyojenga kwa nguvu zao na kukamilishwa na halmashauri baada ya kutokuridhishwa na vioo vilivyowekwa katika madirisha.

Sababu kubwa ya kukataa, kwa mujibu wa wananchi hao, ni kutokana na vioo hivyo kutokuwa na faragha pindi mtoa huduma anapokuwa akimhudumia mgonjwa.

Wananchi hao walisema madirisha hayo hayakukidhi vigezo vya sehemu ya kutolea huduma na yanahatarisha faragha za wagonjwa kutokana na zahanati hiyo kuwa eneo la barabarani.

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Marco Mashene, akizungumza katika mkutano wa hadhara uliotishwa na Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi, alisema vioo hivyo vililetwa kwa ufiicho kwenye zahanati hiyo.

"Walileta vioo hivi nyakati za usiku na muda huo huo fundi alianza kuvipachika bila kukabidhi katika kamati ya ujenzi kwanza na kuvikagua kama vinafaa au la. Tulipomhoji kwa nini anafanya hayo, tulijibiwa kuwa vitakapokataliwa ataviondoa," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema kamati ya ujenzi imevikataa vioo hivyo kwa sababu vinaonyesha mtoa huduma akiwa anatoa huduma kwa mgonjwa, hivyo kunakuwa hakuna siri baina ya mgonjwa, mtoa huduma na wananchi wanaopita jirani na zahanati hiyo, hivyo kuomba viondolewe mara moja.

Akijibu hoja hizo, Mbunge Cherehani alimtaka fundi anayejenga zahanati hiyo kuhakikisha anayaondoa madirisha hayo mara moja na kuweka ambayo yanahitajika kwa mujibu wa sheria kwa kutumia gharama zake.

Mbunge huyo alichangia mifuko 10 ya saruji na maboksi 30 ya vigae kwa ajili ya kukamilisha wa ujenzi wa zahanati hiyo na kuitaka kamati ya ujenzi kusimamia vifaa ili ujenzi ukamilike kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Cherehani alisema maeneo mengi ujenzi unashindwa kukamilika kutokana na kuwepo kwa wizi wa vifaa ambao umekuwa ukifanywa na watu wasio waadilifu, hivyo wale wanaobainika waripotiwe katika vyombo vya sheria.



Sheikh Mfaume Ammari Mwazoa wa Taasisi ya Mustafaa ya jijini Tanga (wa pili kushoto), akitoa mawaidha kwa waumini wa madhehebu ya Shia, wilaya ya Muheza mkoani Tanga juzi, wakati wa kumbukumbu ya kifo cha Imamu Hussein ambaye ni mjukuu wa Mtume Muhammad (SAW), aliyeuawa nchini Iraq mwezi 10 Muharram mwaka 61Hijiria. (watatu kushoto) ni Sheikh Shafi Mohamed Nina wa msikiti wa barabara 20 Tanga mjini. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wananchi 10,000 wafikiwa na huduma ya maji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

ZAIDI ya wakazi 10,000 wa Kijiji cha Bugayambelele, Manispaa ya Shinyanga, wameanza kunufaika na mradi wa maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria, hivyo kuondokana na adha ya kutumia muda mrefu kutafuta huduma hiyo.

Mradi huo unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) umezinduliwa rasmi na Mwenge wa Uhuru na kuwapa fursa wanakijiji hao kuanza kunufaika na maji kutoka katika Ziwa Victoria.

Mmoja wa wananchi hao, Fotunata Malongo, alisema awali walikuwa wakitembea umbali mrefu kufuata maji mjini Shinyanga na wakati wa mvua hutumia maji ya mabwawa ambayo si salama kiafya.

"Mradi huu ni mkombozi kwetu hatutapoteza tena muda wa kufanya shughuli za kiuchumi kutokana na kufuata maji mbali na kijiji chetu," alisema Malongo.

Naye Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Abdalla Shaib Kaim, aliwataka wananchi wanaonufaika na mradi huo kuhakikisha wanatunza miundombinu yake huku akiwasisitiza kuvuta maji katika maeneo yao ili kutekeleza azma ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mbunge wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, aliahidi kuendelea kuomba miradi mbalimbali ya maendeleo huku akiishukuru serikali kwa utekelezaji wa miradi ndani ya jimbo hilo.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa SHUWASA, CPA Sarah Emmanuel, alisema mradi huo utanufaisha wananchi 10,165 na umegharimu Sh. milioni 279.4 mpaka kukamilika kwake.

# Wachimbaji wadogo wakumbushwa leseni

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa dhahabu Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kushughulikia haraka suala la leseni pindi tu wanapogundua maeneo yenye madini. Hali hiyo, imeelezwa kuwa itawasaidia kuzuia migogoro baada ya leseni za maeneo yao kupewa na watu wengine.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake juu ya kuwapo kwa migogoro ya mara kwa mara baina ya wachimbaji wadogo na wawekezaji wenye leseni za uchimbaji madini.

Mhita aliwataka wachimbaji hao kuunda vikundi na kushughulikia leseni ikiwa ni pamoja na kujiendeleza na kupata elimu ambayo itawasaidia katika uchimbaji madini kupitia Tume ya Madini.

Mbali na kuwa mstari wa mbele katika kugundua maeneo yenye madini, alisema wachimbaji wadogo wamekuwa wakiporwa maeneo hayo na watu wenye leseni na kuyabinafsisha hali ambayo inawafanya kukosa maeneo ya uchimbaji na kubaki wakilalamika.

Mkuu huyo wa Wilaya pia alisema sheria kwa kiasi kikubwa inamtambua mtu mwenye leseni na si aliyegundua eneo la uchimbaji na kuongeza kuwa wizara husika inatengeneza mfumo ambao utawasaidia wachimbaji wadogo kuendelea na uchimbaji katika maeneo hayo.

Mbunge wa Msalala, Idd Kassim, alisema wachimbaii wadogo wanapogundua maeneo yenye dhahabu ni bora wakaingia mikataba na watu wenye leseni ya eneo husika ili kuepusha migogoro pale mwekezaji anapotaka kuingia ubia na mtu mwingine.

Alisema Halmashauri ya Msalala na Wilaya ya Kahama kwa ujumla, ina maeneo mengi yenye madini ya dhahabu kwa hiyo ni bora wachimbaji wadogo wasijisahau pale wanapoona kuna mtu mwenye leseni ya eneo hilo na kuingia mkataba naye mapema.

Kassim aliongeza kuwa tayari wameshafikisha malalamiko ya wachimbaji wadogo serikalini na matatizo yao yanafanyiwa kazi ili kuona ni jinsi gani nao wataweza kufaidika na madini pale wanapokuwa wa kwanza kugundua maeneo yenye madini katika sehemu zao.

Alisema katika Halmashauri ya Msalala tayari Rais Samia Suluhu Hassan amekubali kujenga kiwanda cha uchenjuaji wa dhahabu katika eneo la Segese na wachimbaji wadogo watapata fursa ya kupeleka mchanga na kuchenjuliwa kwa gharama nafuu.


Ukurasa 12

**URUSI Vs UKRAINE**
**Kufa kufaana, ndivyo Afrika inavyoelekea kunufaika sasa**


Ukurasa 13

Kinana anapofurahishwa hayupo aliyepinga uwekezaji bandarini


Ukurasa 14

**UCHAGUZI MKUU ZIMBABWE**
**Haya tena 'babu' Mnangagwa na 'dogo' Chamisa ni ngome kuu ya upinzani lakini....**



# Wenyeviti kamati ulinzi, usalama wanapokuwa adui wa wananchi

• Wadau watamani watumbuliwe, washitakiwe sheria ibadilike

**Na Sabato Kasika**

TUME ya Haki Jinai, imeibua sintofahamu nyingi, katika mfumo wakutoa haki kwa wanaofanya makosa ya jinai, miongoni mwake ikiwa ni wakuu wa mikoa, wilaya kujitambulisha kama wenyeviti wa kamati ya ulinzi na usalama katika vituo vyao vya kazi, ikielezwa kuwa si sahihi.

Mwenyekiti wa tume hiyo Jaji Mstaafu Othman Chande, anasema hayo wakati akikabidhi ripoti hiyo kwa Rais Samia Suluhu Hassan, mwezi uliopita na kufafanua kuwa ni kosa kisheria viongozi hao kujitambulisha hivyo.

Katika ufafanuzi wake anasema wakuu hao huambatana na kamati za usalama katika ziara zao, hali inayosababisha hofu kwa wananchi na kushindwa kueleza kero zao kwa kuhofia kukamatwa.

Badala yake, tume hiyo inapendekeza kuwa wakuu wa mikoa na wilaya wanapokuwa wanatekeleza mamlaka ya ukamataji, wazingatie matakwa ya kifungu cha 7 na 15 cha Sheria ya Tawala za Mikoa.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, matakwa hayo ni hadi liwe ni kosa lililotendeka mbele ya kiongozi, liwe la jinai ambalo mtu anaweza kushtakiwa na liwe limesababisha uvunjaji wa amani na utulivu.

Anafafanua kuwa kifungu hicho kinawaelekeza wakuu hao kumuandikia hakimu kumueleza sababu, na kwamba pamoja na kuwapo kifungu hicho, maelekezo hayo hayatekelezwi.

Kutokana na kuwapo kwa mkanganyiko huo, Nipashe inazungumza na wadau mbalimbali wakiwamo wanasheria ili kupata maoni yao kuhusu suala hilo liloibuliwa na tume hiyo.


Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga **PICHA: MTANDAO**

Bob Wangwe ni Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), ambaye anasema namna nzuri pekee inayoweza kuleta msingi wa mabadiliko katika nafasi hizo, ni kuwapo kwa katiba mpya.

"Katiba mpya inaweza kutengeneza utaratibu wa uwajibishaji wa hao viongozi, kwani wamekuwa wakitumia madaraka vibaya, hata ile sheria ya tawala za mikoa inayowapa madaraka ya kuweka watu ndani kwa saa 48, haizingatii taratibu za sheria za serikali za mitaa kama ambavyo hata tume yenyewe imebaini," anasema Wangwe.

Anaeleza kuwa ripoti ya tume hiyo imeonyesha ni jinsi gani ajenda ya katiba mpya inavyoendelea kuzunguka vichwani mwa wapenda demokrasia na watetezi uongozi unaozingatia sheria na utawala bora.

Hivyo, kwa kifupi ni kwamba tuendelee kukazania kuwapo kwa katiba mpya inayotokana na wananchi, ili kuondoa sintofahamu zinazojitokeza katika uongozi," anasema.

**WASHTAKIWE**

Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania CEGODETA, Thomas Ngawaiya anasema wanaotumia nafasi zao vibaya wavuliwe madaraka na kushtakiwa ili kulinda heshima ya taifa.

"Kiongozi anapofanya kosa na likabainika, anavuliwa madaraka anashtakiwa, lakini miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia wengi wakitumia vyeo vyao vibaya lakini hawachukuliwi hatua," anasema.

Ngawaiya anakumbusha kuwa kumweka mtu ndani kwa sababu ya ugomvi wa masuala ya ngono si sahihi, na kwamba baadhi ya viongozi wamekuwa wakituhumiwa na kulaumiwa kutumia madaraka vibaya kwenye eneo hilo.

"Kwa kuwa tumekiri kwamba ni makosa wakuu wa wilaya na mikoa kuitwa wenyeviti wa kamati za ulinzi na usalama, basi ni vyema pia wale wanaotumia nafasi hiyo vibaya waadhibiwe," anasisitiza.

Aidha, Ngawaiya anasema viongozi hao kuwa wenyeviti wa kamati za ulinzi na usalama kwa imani kuwa wanaweza kujua wakorofi na hatari katika maeneo yao na kuwapa taarifa polisi ili wakamatwe.

"Lakini badala yake, wengine wamekuwa wakitumia nafasi hiyo vibaya, yaani kiongozi anagombania mapenzi na raia, anamuweka ndani hata zaidi ya saa 48 kisha anamwachia," anasema licha ya kwamba hakuwa na ushahidi.

Ngawaiya anasema viongozi wa aina hiyo hutakiwa kuvuliwa madaraka na kuadhibiwa kama wanafanya bila kushirikisha serikali ili iwe fundisho kwao na kwa wengine ambao watakuwa wana nia ya kwenda kinyume na utawala bora.

**NAFASI ZIFUTWE**

Dokta Anna Henga, ni wakili na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC). Anasema ni wakati sahihi kufuta nafasi hizo za uenyekiti wa kamati za ulinzi na usalama.

"Kwa muda mrefu baadhi yao wamekuwa wakitumia vibaya nafasi hizo kwa manufaa yao au ya chama na kusababisha migogoro isiyo ya lazima kwenye jamii, kwa manufaa yao au ya chama," anasema

Dk. Anna anafafanua kuwa hawana mafunzo ya usalama na kukamata raia ni wanasiasa tu, na kwamba tume imebaini hayo kwa kuwa sheria ya jinai haiwatambui kuwa na vyeo hivyo.

"Ingawa zipo baadhi ya sheria zinazotambua cheo hicho, hivyo ni vyema serikali ikapeleka muswada bungeni hata Septemba mwaka huu, ili sheria hizo zirekebishwe, wasiwe wenyeviti wa kamati hizo kwani utendaji wa baadhi yao umekuwa ukilalamikiwa," anasema.


"Pamoja na hayo, vyombo vinavyohusika na haki jinai, ni muhimu vikaanza kutekeleza mapendekezo ya tume, hasa yale yasiyohitaji matumizi ya fedha au kubadilisha sheria," anasema.

Vilevile Mkurugenzi Mtendaji Anna, anasema anatamani wadau wa haki jinai washirikiane na serikali kutoa elimu kwa wananchi ya umuhimu wa kutii sheria bila shuruti ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima na vyombo vya dola.

URUSI VS UKRAINE

# Kufa kufaana, ndivyo Afrika inavyoelekea kunufaika sasa

## •Mkutano wakuu unapoibua mkakati kutokomeza njaa



Viongozi wa Afrika katika mkutano wa pamoja na Rais wa Urusi Vladimir Putin, (kushoto).**PICHA: MTANDAO**

**Na Nimi Mweta**

WAKATI vita vya Urusi na Ukraine vikisababisha Urusi kuwa na maadui wengi wanaoongozwa na Marekani na Ulaya, Afrika imejisogeza karibu na Mrusi ambaye sasa anaahidi kuifanya kuwa mzalishaji mkubwa wa nafaka, kumaliza njaa na hata kuuza nje.

Yanajiri wakati wa mkutano wa viongozi wa Afrika na Rais Vladimir Putin wa Urusi, uliofanyika jijini St. Petersburg, katika mazingira tofauti na yale ya mkutano uliotangulia, Oktoba 2019 huko Sochi.

Kufanya mkutano huo kwenye jiji hilo la kizamani kuna maanisha kuwa kuna ukata kwa vile Sochi ni eneo la kitalii, burudani tena na kimichezo tofauti na St. Petersburg, mji mkongwe na wa kihistoria.

Kilimo cha nafaka kinakuja baada ya kipindi cha awali Urusi kutoa 'ofa' ya msaada wa takriban tani 20,000 kwa nchi kadhaa za Afrika zenye upungufu wa chakula bila malipo, kwa miezi mitatu.

Mataifa hayo ni pamoja na pamoja na Mali, Somalia na Eritrea, wakati Rais Emmerson Mnangagwa wa Zimbabwe akipewa zawadi ya helikopta ya kutumia kufanya kampeni katika uchaguzi mkuu unaofanyika mwezi huu.

Bado kuna hatua nyingine ambayo inangojewa barani hapa ya kuunda ubia ambako mataifa ya Afrika yanatoa ardhi na Urusi au washirika wengine kutoa vifaa, teknolojia na kusimamia uzalishaji wa ngano badala ya kuhitaji kuinunua kutoka nchini humo, walipwe kwa fursa nyinginezo kama mafuta, madini na madini adimu.

Kimsingi kuunda mikakati kama hiyo ni kutatua matatizo ambayo hayana majawabu katika soko, kwani wazalishaji hao au watoa fedha na vifaa hawawezi kukutana sokoni, au katika maonyesho ya kilimo, na kuunda wazo kama hilo.

Ni hatua zinazohitaji kuchukuliwa na serikali za Afrika, watoe motisha kwa watakaoonekana wanaweza kufanya shughuli kama hiyo.

Pale watu kama hao wanapojua kuwa ni serikali zinataka kazi hiyo ifanyike watazuia ubabaishaji, kwani muda mwingi miradi inakwama wahusika wakianza kuvutana.

Hiyo pia ina maana ya kurekebisha kiasi fulani diplomasia ya uchumi, kutoka kwenye kutangaza vivutio na kwenda kwenye utafutaji wa kampuni kufanya shughuli fulani. Siyo suala la kutangaza zabuni za kimataifa kwani watakaojitokeza mara nyingi wanataka faida ya haraka haraka badala ya mpango endelevu, halafu wanaopitia maombi hayo wanataka 'wakunje mkwanja wa haja' kwa bahati hiyo.

Matokeo yake ni mivutano ya kisheria na hata kisiasa watu wakitupiana mpira tatizo lilikuwa wapi, lengo kwa jumla lisifanikiwe.

Siyo rahisi kuhakikisha kuwa hapatakuwa na makosa yoyote katika uwekezaji na uendeshaji wa miradi mikubwa ya kuzalisha nafaka hasa kwa kuuza nje.

Ila kampuni zilizosimama vizuri kibiashara na zenye malengo ya kitaifa na siyo tu ya faida binafsi za kampuni au wakurugenzi wake, inatoa picha nzuri zaidi ya uwezekano wa miradi kama hiyo kufanikiwa, kwa vile hakuna uwezo wa kufikia ngazi ya kuuza nafaka kwa wingi nje kwa kutumia soko.

> Hata hivyo kuna uwezekano kuwa kutokana na athari hizo na kulemewa zaidi na mabadiliko ya tabianchi, wakuu wa nchi za Afrika wanamsikiliza Rais Putin shingo upande.

**UWEKEZAJI NISHATI**

Yanayozungumzwa ni mengi lakini Rais Yoweri Museveni wa Uganda katika mkutano huo anakumbusha pia umuhimu wa kupanua utafutaji mafuta na gesi Afrika, kuwa Urusi iweke nguvu au mkazo zaidi katika eneo hilo.

Anasema makundii yenye ushawishi mkubwa nchi za Magharibi yanapiga vita kutafuta na kuchimba au kusafirisha mafuta. Ina maana pia wanataka Urusi, China na baadhi ya marafiki wengine waelewe.

Wakati suala hilo halijaangaliwa kwa undani, inawezekana kuna mabadiliko ya kimsingi katika mahusiano ya Afrika na nchi za nje, kutokana na maeneo mihimili ya sera za nchi za Magharibi kwa Afrika, yaani demokrasia na kuondoa nishati za makaa ya mawe na mafuta, ila gesi kwa uchache zaidi.

Urusi yenyewe ni muuzaji mkubwa wa mafuta, ila tatizo la Afrika siyo soko la hayo mafuta kwani bado lipo na inaelekea litaongezeka, licha ya juhudi za kufikia nishati mbadala katika nchi tofauti kila kukicha.

Suala hasa ni kupatikana mitaji ya kufanya shughuli hizo, kama wawekezaji na wadau kutoka nchi za Magharibi hawataki.

Ina maana kuwa mkanganyiko wa kiuchumi duniani kutokana na vikwazo vya nchi za Magharibi kwa Urusi na jitihada zao kupunguza utegemezi wa sekta muhimu hasa TEHAMA kwa waathirika kiteknolojia au soko nchini China, ni fursa nyingine kwa Afrika. Hilo linajitanua ndani ya hali ngumu zaidi ya kidiplomasia ambayo hata hivyo Afrika inaonyesha kuwa iko tayari kuwa sehemu ya sintofahamu inayoenea, kuwa kuongea na Magharibi na mahasimu wake kwa pamoja.

Ila tatizo la kutoweza demokrasia linaunganisha nchi za Afrika na Urusi au China na wengine kwa nguvu zaidi, ili wasiulizwe kuhusu hoja hiyo.

Inaelezwa kuwa idadi ya viongozi wakuu walioshiriki ilipungua, sababu muhimu ikiwa ni kutofurahishwa na vita vya Ukraine na athari zake kwa mataifa ya Afrika.

Hata hivyo kuna uwezekano kuwa kutokana na athari hizo na kulemewa zaidi na mabadiliko ya tabia nchi, wakuu wa nchi za Afrika wanamsikiliza Rais Putin shingo upande.

Kwa baadhi ya wachambuzi wa hali ya kisiasa na kiuchumi katika Afrika, kuna tofauti kati ya mikutano hiyo kutokana na kuwa dhamira ya Urusi na mbinu zake iko wazi zaidi sasa, siyo tu kutokana na Ukraine ila hata uwepo wa kundi la kijeshi la Wagner linaloweza kuajiriwa au kukodishwa na nchi yoyote.

Kwa mfano taifa likihitaji wapiganaji dhidi ya makundi ya siasa hali yaliyotapakaa kwenye nchi za KUsini ya Jangwa la Sahara na Afrika Mgharibi.

Kundi la Wagner linaonekana kuwa jawabu linalopendwa zaidi na nchi hizo, kuiondoa Ufaransa.

Hali hiyo imejitokeza wakati mkutano wa wakuu wa nchi za Afrika na Urusi ukiendelea huko St. Petersburg, kikosi maalum cha ulinzi wa Ikulu ya Niamey nchini Niger wakamzuia Rais Mohamed Bazoum na kutangaza utawala mpya, ukiitwa ni wa mpito.

Hawakufanya juhudi halisi ya kutoa ahadi ya lini wataachia madaraka, serikali iliyopinduliwa ndiyo kwanza ilitimiza miaka miwili Aprili, hivyo suala la 'kuihukumu' mapema hivyo ni kama inapingwa,

Kushindwa kusikilizia zaidi ina maana mifumo ya kisiasa kwa jumla imeshindwa na vikosi hivyo vinataka majibu mengine, si uchaguzi.

Tukio hilo lilileta kitu kama shangwe katika miitikio ya baadhi ya wadau na hasa huko Urusi ambako kundi la Wagner au wadau wake wa karibu waliita tukio hilo kama la kurejesha uhuru wa nchi.

Ina maana nchi za Magharibi zinalazimisha uchaguzi ambako viongozi wasiofaa wanashinda, wazo ambalo haliko mbali sana na makundi ya vijana ambao wamekuwa wakiandamana kushinikiza mapinduzi ya kijeshi katika nchi kama Mali, Burkina Faso, Afrika ya Kati, Guinea na sasa Niger.

Mojawapo kati ya makundi ya vijana walibeba bango linalosema 'tunataka utawala wa mpito wa miaka 10,' ambayo inaweza kutafsiriwa kuwa ni uhusiano wa kudumu na mataifa kama Urusi ili kusafisha magaidi.

Kimsingi watawala wa Urusi na kundi la Wagner wako tayari kwa kazi hiyo, alimradi wanakuwa huru kuendesha shughuli za kutafuta madini adimu hasa kwa mahitaji ya nishati endelevu maeneo mengi duniani.

# Kinana anapofurahishwa hayupo aliyepinga uwekezaji bandarini

**Na Beatrice Shayo, MARA**

WATANZANIA wameongea wapo wanaoutetea, wanaoupinga na wanaoukosoa mkataba wa uwekezaji lakini hakuna anayesema kusiwe na mwekezaji bandarini.

Inavyoelekea wanakubali haja ya kuwekeza na lengo ni ufanisi na mapato zaidi katika lango hilo la kiuchumi, anasema, Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana.

Anatoa uchambuzi huo kwenye mkutano wa hadhara mkoani Mara unaofanyika viwanja vya Mkendo Musoma mjini, akiwa kwenye ziara ya kukagua miradi ya maendeleo na utekelezaji wa ilani.

Mwezi uliopita Kinana anazitembelea wilaya za Kondoa mkoani Dodoma, Babati, Manyara, Mara, Simiyu na Tabora akiongozana na baadhi ya wajumbe wa Halmashauri Kuu (NEC), kuangalia utekelezaji wa ilani.

Anasema jambo la bandari limechukua mjadala mkubwa umefika mahali unawachanganya wananchi na kuwagawa kwa sababu kila mmoja anaeleza lake.

Anaeleza kuwa serikali itakwenda kufanya kazi kwa nia njema ya kuongeza ufanisi na mapato ili kufanya shughuli nyingi zaidi za maendeleo.

Kinana anasema waliojitokeza kuhoji, wapo wanaohoji kwa nia moja ya uzalendo na hawawezi kueleza kila anayehoji ana nia mbaya.

"Wapo ambao wanapitia mkataba wametoa ushauri mzuri, serikali itapokea kila ushauri utakaotolewa na CCM imeagiza isikilize maoni na ushauri wa wananchi. Inasikiliza ushauri, maoni na hoja zinazotolewa na hofu zinazotolewa pia haya yote yatafanyiwa kazi," anasema Kinana.

YANAFANYIWA KAZI

Anaongeza kuwa Rais Samia Suluhu Hassan, anayafanyia kazi maoni yaliyotolewa na haiwezekani Rais Dk. Samia akapuuza maoni ya wananchi ndiyo maana amemuona tangu mjadala umeanza amekaa kimya anayafanyia kazi.

Anasema kiongozi bora panapotokea mambo ambayo kuna ubishi na hoja mbalimbali sio yule anayejaribu kujibu kila hoja inayosemwa.

Kinana anasema mzuri ni yule aliyetulia, alichokifanya Rais Samia ni kuwa mtulivu na kusikiliza kila hoja, kuchambua na kutathimini kila moja ili muda utakavyofika wapate uwekezaji ulio bora zaidi kwa manufaa ya Tanzania.

**KUACHA CHUKI**

Kinana anawataka watu kuhoji kwa utaratibu bila kuweka chuki, akisema wapo waliosema kwa hisia kali, waliopeleka mjadala huo kwenye masuala ya muungano na udini hapakuwa na sababu kwani uwekezaji huo ni wa kiuchumi inatakiwa kujadiliwa kwa hoja ambazo zitasikilizwa.



Kinamama wakimfurahia na kumpongeza Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara Abdulrahman Kinana. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

"Hoja zitafanyiwa kazi kwa maslahi ya nchi hakuna anayekataa uwekezaji. Serikali inaendelea kusikiliza maoni na hofu zinazotolewa na chama chetu kimeagiza wananchi wasikilizwe kwa kila ngazi na kila sehemu na serikali inaendelea kufuatilia,"anasema Makamu Mwenyekiti.

Anasema, hata Rais Samia alivyofikia uamuzi wa kuwekeza katika bandari ni kwa sababu ya jambo moja la maslahi ya Watanzania na nchi na sio kwa sababu yoyote.

'Najua tupo watu wengi, vyama vingi ndiyo wakati muafaka likitokea jambo kila mmoja anatafuta namna ya kulitengeneza kwa namna ambayo inakuwa na manufaa kwao kwa hiyo ukipiga kelele kwa kueleza imeuzwa, ningependa Watanzania waamini haijauzwa hakuna bandari inayouzwa,' anasisitiza.

Kinana anahoji bandari inauzwaje? Na ni kwa nini iuzwe hapa bandari ya Musoma imeuzwa? Kwa bei ipi? Ili iweje hakuna sababu na kuwaomba watu wawe watulivu na imani na Rais kwa kuamini kwamba kila jambo analolifanya lina maslahi na taifa.

Anasema Rais Samia aliyekula kiapo hawezi kufanya jambo ambao halina maslahi na nchi yake amefanya mambo mbalimbali ya kimaendeleo, kwa nini aende kuuza bandari kwa sababu zipi? Ili apate nini, ili iweje? ukiusikiliza huo mjadala msikilize kwa umakini.

**AONYA WABUNGE'**

Aidha, Kinana anawataka wabunge na madiwani kabla ya kupitisha sheria wahakikishe wanachukua mawazo ya wananchi na kuyafanyia kazi badala ya kupitishia sheria kandamizi ambazo umma hauzifahamu.

"Muache tabia ya kujifungia kwa kutafuta mapato kwa kutunga sheria ambazo zinakwenda kuumiza wananchi na badala yeke wawashirikishe wananchi na sio kutunga sheria kandamizi,"anasema Kinana,

Anaongeza:"Madiwani mpo hapa mnapokuwa mnatengeneza sheria za halmashauri na serikali za mtaa tengenezeni sheria rafiki kwa wananchi msijifungie mahali mnatafuta mapato, hamna habari kwamba sheria hizo zinakwenda kuumiza watu,".

Kinana anawaeleza kuwa kabla hawajatunga sheria wajue umuhimu wa kuwashirikisha wananchi kwa sababu wametoka katika kata hizo na endapo wakidai sheria hiyo ni mbovu ziondolewe.

Anawakumbusha kuwa wananchi hao ndiyo wapiga kura wao kwa nini hawapewi heshima ya kuulizwa katika sheria hizo na badala yake zinageuka kuwatesa.

"Tukitunga sheria hatuwaulizi wananchi na hata hao wapigakura hawazijui wakikamatwa ndiyo wanaambiwa sheria ambayo haijui. Sio sawa, madiwani na wabunge kama sheria imeletwa na wanaona haina maslahi na wananchi ni bora wakaiache ,"anasisitiza Kinana.

Anasema, katika kuzisimamia kuna sheria, kanuni na taratibu na jambo lazima liende na utekelezaji wa sheria ambalo ni busara si kila kitu ni sheria.

"Si kila wakati ni kamata weka ndani kwani nyinyi hamjui kusamehe sheria yenu haina kifungu cha kusamehe ni adhabu peke yake mtu anachukua shughuli yake ndogo ameweka mahali anauza anakamatwa vitu vyote vinakusanywa na kuchukuliwa na mtaji unaishia hapo,"anawaeleza Kinana.

Anasema mtu anapokuwa amevunja sheria ajulishwe ukweli wake kuhusiana na kosa lake na aelezwe hairuhusiwi na kumpa onyo badala ya kumkimbizia kituo cha polisi wakati anahitaji kuelimishwa.

**KUBADILI VIONGOZI**

Makamu Mwenyekiti Bara, akiwa wilaya ya Kondoa Mkoa wa Dodoma , anazungumza kwenye mkutano wa hadhara anapoeleza kuwa hakuna sababu ya wananchi kubadilisha viongozi kama mashati jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo.

Kinana anasema ni muhimu kwa wananchi kujenga tabia ya kutobadilisha viongozi wao kama mashati endapo hakuna ulazima wa kufanya hivyo.

"Kila binadamu ana kasoro, hakuna mkamilifu, lakini wananchi hususani wapigakura wasimuadhibu mtu kwa mambo madogo badala yake waangalie kazi kubwa na mazuri anayoyafanya mfano ni haya majimbo yote ambayo wabunge wake hawabadilishwi kama mashati yamepiga hatua kubwa kwenye maendeleo,"anasema Kinana.

Anafafanua kuwa inawezekana mbunge asifanye kila kitu kwa ukamilifu naye ni binadamu na anaweza kuwa na kasoro, lakini ukitaka kuishi na mwenzako vizuri tafuta mema yake usifuatilie upungufu wake muda wote.

"Tunavyoishi ukitafuta upungufu wa mtu mtakosana ukizungumza mema yake mtaishi pamoja kila binadamu ana upungufu hata mimi nina yangu. Na yeye atakuwa anajua upungufu wao lakini yote yanawekwa kando na kutafuta mema na kufanya maisha kuwa mema zaidi,"anasema Makamu Mwenyekiti Bara.

Kiongozi huyo anasema katika kufanikisha maendeleo yoyote ni lazima kuwepo umoja na mshikamano, kwani mambo hayo yakikosekana maendeleo yatakuwa hafifu kwa sababu viongozi na wananchi watakuwa wakibisha katika kila jambo.

"Mnataka kuweka mradi wa maji mnabishania uende wapi, mnataka kujenga shule mnasema ijengwe wapi, mnabishana hadi fedha zinarudi serikali kuu. Mnataka kuamua nyumba za walimu zijengwe wapi hamkubaliani. Mkiwa na umoja maendeleo yatakuwa ya haraka zaidi,"anasema Kinana.

UCHAGUZI MKUU ZIMBABWE

# Haya tena 'babu' Mnangagwa na 'dogo' Chamisa ni ngome kuu ya upinzani lakini....

**Na Gaudensia Mngumi**

WAZIMBABWE sasa ni mguu sawa.Wanaelekea kwenye boksi la kura, uchaguzi wa Rais na bunge baadaye mwezi huu, si mbali ni hapo Jumatano Agosti 23. Unakuwa wa mara ya pili tangu kuondolewa madarakani kwa mpigania uhuru mkongwe jongwe Robert Mugabe.

Kama kawaida,zilivyo nchi nyingine za Afrika kuna wagombea lukuki wapo11 wanaowania kiti cha urais. Hata hivyo, mchuano mkali ni kati ya Rais anayemaliza muda wake Emmerson Mnangagwa (80) kutoka chama tawala cha ZANU-PF na Nelson Chamisa (45), wa chama cha upinzani cha Citizen's Coalition for Change (CCC).

Chamisa katika uchaguzi wa 2018, aliibuka wa pili na kujinyakulia asilimia 44 ya kura. Uamuzi wa mahakama wa 2020 ulimvua uongozi wa chama kikuu cha upinzani cha wakati huo cha Movement for Democratic Change (MDC) na baadaye akapoteza uwezo wa kupata mali za chama na ufadhili wa serikali.

MDC ilianzishwa na Morgan Richard Tsvangirai. Sasa marehemu alikuwa mwanasiasa wa upinzani Zimbabwe aliyewahi kuwa Waziri Mkuu kuanzia 2009 hadi 2013, akiongoza serikali pamoja na Mugabe.

Hakupoa mwaka 2022 aliunda CCC na bado ni maarufu sana katika maeneo ya mijini na ndiye sura kuu ya upinzani katika uchaguzi huo..

Wagombea wengine ni pamoja na Douglas Mwonzora, kiongozi mpya wa MDC na Elisabeth Valerio, mgombea pekee mwanamama.

Mnangagwa, mkuu wa ujasusi wa zamani ambaye alichukua hatamu baada ya kiongozi wa muda mrefu Robert Mugabe kupinduliwa katika mapinduzi ya kijeshi ya mwaka 2017, anawania muhula wa pili, ni baada ya kumshinda Chamisa katika uchaguzi uliofanyika 2018.

Wachambuzi wa masuala ya kisiasa wanasema kinyang'anyiro hicho kinawapa ushindi upande wa Mnangagwa na ZANU-PF, ambayo imeiongoza Zimbabwe tangu mwaka 1980 na inaonekana itatumia vibaya udhibiti wake wa taasisi za serikali zikiwamo polisi na vyombo vya habari ili kujibakisha madarakani.

Vyombo vya habari vya serikali vinatoa muda mchache kwa upinzani, na polisi mara kwa mara husimamisha mikutano yake ya kampeni.

Chama cha CCC cha Chamisa kinatumia karata ya kuchanganyikiwa na kuongezeka kushindwa kwa ZANU-PF katika kushughulikia uchumi kutasaidia kuinua kiwango chao kwa wananchi kikiunga mkono na hata kupata ushindi.



Nelson Chamisa –CCC



Rais Emerson Mnangagwa ZANU –PF

**YANAYOTAZAMWA**

Katika uchaguzi huo mambo makuu ni pamoja na uchumi kuendelea kutetereka, ukisalia kuwa suala kuu na pasua kichwa katika Zimbabwe yenye utajiri wa madini kupindukia.

Huenda watu walikuwa na matumaini kwamba nchi ingereje na maisha kuimarika chini ya Mnangagwa, lakini mambo yalififia haraka na kuwaacha wananchi wakikabiliana na uhaba mkubwa wa umeme na kupanda kwa bei za bidhaa.

Aidha, mfumuko wa bei wa mwaka hadi mwaka ni changamoto kwani kuna wakati ulifikia asilimia 557 nayo ni Juni 2020, wakati huu uko juu kwa asilimia 74.5 na pia kilifikia kipindi Zimbabwe ilikuwa taifa kati ya nchi zenye mfumuko wa juu zaidi duniani.

Dola ya Zimbabwe, iliyorudishwa tena na Mnangagwa mwaka 2019 baada ya muongo wa dola ya Marekani, imeshuka kwa zaidi ya asilimia 80 mwaka huu.

Itakumbukwa kuwa Dola ya Zimbabwe ilisimama kutumika mwaka 2009 na nafasi yake ikachukuliwa na Dola ya Marekani ikiwa ni hatua za kudhibiti mfumuko wa bei. Aidha, baada ya kipindi kirefu cha mfumuko wa bei klichoifanya sarafu hiyo kukosa thamani, ilirejeshwa tena katika jaribio la kufufua uchumi uliodorora na Rais Mnangagwa..

Ukosefu wa ajira umebaki kuwa wa juu sana, suala muhimu la uchaguzi kwa vijana walio na umri wa chini ya miaka 35, ambao ni asilimia 70 ya watu wote.

**UJUMBE WA WAGOMBEA**

Rais Mnangagwa, ambaye hotuba zake za kampeni mara nyingi huongozwa na maelezo ya utaifa yanayokumbusha harakati za kupigania uhuru wa Afrika, anasema serikali yake imetoa fursa kwa wazawa katika uchumi na sera zinazounga mkono ushiriki wao katika sekta kama vile madini na kilimo.

Chamisa, kwa upande mwingine, anasema sera za Mnangagwa zinawapendelea wasomi wachache waliojiunganisha na serikali. Anaahidi kuwa akishinda atakuza uchumi, kupambana na ufisadi na kukomesha kutengwa kwa kuwekewa vikwazo Zimbabwe na jumuiya ya kimataifa.

Anaahidi kuwa serikali ya CCC itaweka nidhamu ya fedha na matumizi ya umma, kurejesha heshima ya haki za binadamu na mali na kuvutia uwekezaji.

**WAPIGAKURA 2023**

Takriban watu milioni 6.6 wamejiandikisha kupiga kura katika uchaguzi wa mwaka huu, wakati milioni 5.7 walijitokeza mwaka wa 2018, tume ya uchaguzi ya nchi hiyo inasema.

Ili kushinda urais, mgombea lazima apate zaidi ya asilimia 50 ya kura. Ikiwa hakuna mshindi wa moja kwa moja, uchaguzi unarudiwa na utafanyika Oktoba 2.

Kwa upande wa wagombea ubunge na udiwani wanahitaji kura nyingi zilizopigwa kushinda na hakuna kigezo zaidi.

Licha ya idadi kubwa ya watu wanaoishi nje ya nchi, wengi wao wakiwa katika mataifa jirani ya Afrika Kusini na Msumbiji, Zimbabwe hairuhusu raia wake kupiga kura wakiwa kwenye mataifa jirani.

Kwa mujibu wa sheria za uchaguzi za Zimbabwe matokeo ya uchaguzi wa urais lazima yatangazwe ndani ya siku tano baada ya upigajikura kukamilishwa.

**MITANDAO**



HABARI DODOMA

## Taarifa za wenye ulemavu sasa kukusanywa kidijitali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inatarajia kuanzisha mfumo wa kielektroniki utakaowezesha kukusanya taarifa za watu wenye ulemavu.

Mfumo huo pia unatarajiwa kuwezesha kusajili, kuratibu, kusimamia na kufuatilia masuala na huduma zinazohusu watu wenye ulemavu.

Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa Ofisi hiyo, Fatma Mgembe, alibainisha hayo jana alipotoa elimu kwa umma kuhusu mfumo huo jijini hapa.

Alisema lengo la kuanzishwa mfumo huo utawezesha upatikanaji wa uhakika wa taarifa za watu wenye ulemavu, kutambua aina ya ulemavu, mahitaji na idadi yao, kujua vyanzo vya ulemavu na kuwa na mipango thabiti ya kutoa huduma.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa ofisi hiyo, Gerold Komba, alisema mfumo huo ni sehemu ya uboreshaji rejesta ya watu wenye ulemavu ili kuongeza ufanisi katika utendaji na uchambuzi wa taarifa zao.

Alitoa rai kwa wazazi na walezi kutoa ushirikiano kwa watendaji watakaokuwa wanakusanya taarifa hizo ili watu wenye ulemavu wasajiliwe katika mfumo huo, utakaowezesha serikali kutekeleza hatua endelevu kwa ustawi.

**Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wa Ofisi hiyo, Fatma Mgembe, alibainisha hayo jana alipotoa elimu kwa umma kuhusu mfumo huo jijini hapa.**

# Waliopandizwa uume waonyesha matokeo chanya, gharama Mil. 6/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HUDUMA ya upandikizaji uume iliyofanywa kwa wanaume wawili waliokuwa na tatizo la nguvu za kiume katika Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) jijini Dodoma, imeonesha matokeo mazuri na 'heshima' imerejea kwa familia zao, huku gharama zake zikiwa kati ya Sh. milioni sita hadi 10.

Akizungumza jana jijini hapa na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya hospitali hiyo na mwelekeo wake kwa mwaka wa fedha 2023/24, Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Dk. Alphonce Chandika, alisema huduma hiyo imeanzishwa baada ya kubaini kuna tatizo kubwa la nguvu za kiume.

"Tumeona hata wenzetu waganga wa kienyeji wanapita huko mtaani kule na dawa ya kutibu tatizo hili. Wananchi wanasumbuka, sisi kama taasisi ya umma tumeona tuje na mkakati wa kuwasaidia wananchi.

"Tulianza kutoa huduma mwezi Juni 2022 kwa wanaume wawili, lakini kwa habari njema kutoka kwao mambo ni mazuri.

"Mambo ni mazuri sana kwa sababu tuliwapa masharti wakae wiki sita ndipo waanze kujaribu mitambo, mitambo imekaa vizuri na wao wametuambia matokeo mazuri wamefurahi sana na imerejesha heshima katika familia zao," alisema.

Alibainisha kuwa wako katika mchakato wa kuongeza wigo wa utoaji huduma ili zipatikane kwa wahitaji wote na wale wanaotengeneza vipandikizi wanakamilisha taratibu za usajili ili kufungua ofisi Dar es Salaam itakayorahisisha upatikanaji wake.

"Ninatumaini baada ya kuanza sisi na hospitali zingine zitatoa kwa kuwa uhitaji ni mkubwa. Sisi pekee yetu hatutotosheleza. Kwa hiyo, tutashirikiana na wenzetu hata kuwapa mafunzo ili watoe huduma katika hospitali zao," alisema.

Kiongozi huyo alisema gharama siyo kubwa kulinganishwa na tabu anazopata mtu mwenye tatizo hilo. Ni kati ya Sh. milioni sita na 10.

Alisema magonjwa ya kisukari na shinikizo yanachangia kwa kiasi kikubwa tatizo la nguvu za kiume na kuwashauri wananchi kujiepusha na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

"Pia nitahadharishe kuhusu mitindo ya kujamiana ambayo imeonekana kuchangia tatizo hili kama mlivyosikia kuna mmoja wa wagonjwa ilitokana na mitindo hiyo (sehemu zake za siri zilivunjika). Sasa inawezekana kuna wengine huko wengi mtaani, hivyo nitoe tahadhari," alisema. Kuhusu upandikizaji figo, kiongozi huyo alisema kwa mwaka uliopita wananchi wanane walinufaika na upandikizaji figo na wametumia Sh. milioni 288.

Kama wangepelekwa nje ya nchi kupata huduma hiyo, wangetumia Sh. milioni 600 kulingana na gharama za hospitali za nje, hivyo kwa huduma hiyo serikali imeokoa Sh. milioni 312.

"Katika huduma za matibabu ya moyo tumeendelea kuimarika. Mwaka uliopita tumefanya uchunguzi wa mishipa ya moyo kwa wagonjwa 320, upandikizaji betri wagonjwa 13, watoto waliozibwa matundu katika moyo 14, kuweka vizibua njia ya mishipa ya moyo 54, huduma ya vipandikizi katika magoti na nyonga wananchi 72 wamenufaika na huduma hii na serikali imetumia Sh. milioni 864 na kama wangeenda kupata huduma hii nje ya nchi, ingeigharimu serikali Sh. bilioni 2.5, hivyo Sh. bilioni 1.638 zimeokolewa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa katika huduma ya upandikizaji uloto, imekuwa na manufaa makubwa kwa watoto wanne ambao wamepona kabisa na huduma hiyo inapatikana Hospitali ya Benjamin Mkapa kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati kwa gharama za matibabu Sh. milioni 50 wakati matibabu hayo nje ya nchi yanagharimu Sh. milioni 120 hadi 135.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2023/24, wametenga Sh. bilioni 64.52. Kati yake, Sh. bilioni 18.62 ni za miradi ya maendeleo ili kuendelea kuwapunguzia wananchi adha ya kusafiri mbali kupata matibabu.

Alisema miradi yao inajumuisha ujenzi wa kituo cha upandikizaji wa figo chenye vyumba vya upasuaji kwa anayechangia figo na anayepokea.



Mkuu wa mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule akizungumza na waumini wakati wa ibada maalumu ya kumshukuru Mungu kwa serikali kuwekeza miradi mikubwa kwa ajili ya maendeleo ya watanzania, katika Kanisa la Karmeli Assemblies of God Ipagala, Dodoma juzi. **PICHA PETER MKWAVILA**

# CCM yaagiza kufanyika uchunguzi hofu ubadhirifu ujenzi kituo cha afya

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimemtaka Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, kuunda kamati ya kuchunguza hofu ya ubadhirifu katika mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Unyambwa, Manispaa ya Singida ambacho serikali ilitoa Sh. milioni 500.

Imeelezwa kuwa fedha zote zimeshatolewa, lakini ujenzi haujakamilika.

Katibu wa CCM Wilaya ya Singida Mjini, Shaban Hamis, alitoa rai hiyo juzi wakati wa kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa kilichoitishwa kwa lengo la kujadili utekelezaji wa ilani.

"Katika sekta ya afya, hali ni mbaya, vituo vingi vya afya havijakamilika vikiwamo vinavyojengwa kwa nguvu za wananchi. Mfano, Kituo cha Afya Unyambwa ujenzi wake umesimama kwa miaka miwili. Tukienda hivi tunaweza kukosa kura 2024," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Serukamba, alikili kuwa, baadhi ya vituo vya afya havijakamilika. Wakati ujenzi wa Kituo cha Afya Unyambwa unaanza hakuwa Mkuu wa Mkoa.

Akaweka angalizo siyo kweli kwamba hali ya afya ni mbaya kama inavyoelezwa kwa kuwa suala la afya lina mambo mawili - utoaji huduma na majengo. Katika utoaji huduma hali ni nzuri.

Tamko hilo la Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa limetolewa ikiwa ni siku mbili baada ya wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa kutoa agizo kwa viongozi wa serikali wilayani Singida kuchukua hatua za kisheria haraka dhidi ya watumishi waliosimamia ujenzi wa mradi wa kituo hicho cha afya.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida, Martha Mlata, aliagiza hayo akiwa na wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa walipotembelea na kukagua mradi huo na kubaini ujenzi umekwama kuendelea kwa miaka miwili sasa kutokana na fedha zilizotolewa na serikali kuisha.

Wajumbe wa kamati hiyo walielezwa kuwa Manispaa ya Singida katika mwaka huu wa fedha imelazimika kutenga Sh. milioni 90 kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa kituo hicho.

Martha alihoji kama Mkuu wa Wilaya ya Singida aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza utata wa matumizi ya fedha hizo na sababu za uchunguzi huo kuchukua miaka miwili bila kukamilika.



# Waliotorosha mwanafunzi ili aolewe wakamatwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kumtorosha mwanafunzi wa shule ya sekondari na kutaka aolewe na kijana wao kinyume cha sheria.

Wanaoshikiliwa ni Nazareth Ndele (50), Steven Mwaigaga (29) na Faraja Mwaigaga (26), wote wakazi wa Kijiji cha Igundu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi, Benjamin Kuzaga, alisema watuhumiwa hao walikamatwa Julai 27, mwaka huu, walipokwenda nyumbani kwa mzazi wa binti huyo kutoa mahari.

Kamanda Kuzaga alisema binti huyo mwenye umri wa miaka 17 alipangishiwa nyumba jirani na shule kutokana na nyumbani kwao kuwa mbali.

Alisema Julai 20, mwaka huu, kijana aitwaye Chande Mwaigaga alimfuata binti huyo kwenye nyumba aliyokuwa anaishi na kuondoka naye kwenda kuishi katika Kijiji cha Ilindi, kama mume na mke.

"Kijana huyo alianza kumshawishi mwanafunzi huyo ambaye jina tumelihifadhi walipokutana Juni 12, mwaka huu, huko katika Kijiji cha Santilya, alimshawishi na kuingia naye kwenye uhusiano wa kingono," alisema Kamanda Kuzaga.

Alisema Julai 27, 2023 saa 3:00 asubuhi, baba mzazi wa mwanafunzi huyo, Majaliwa Miston (46), akijua mwanaye yuko shuleni alipokea wageni watatu ambao ndiyo watuhumiwa wakijitambulisha kuwa ni washenga wa Chande.

Kamanda Kuzaga alisema baba mzazi wa binti huyo alipowahoji walijibu kwamba binti yake anaishi na kijana anayeitwa Chande Mwaigaga na wakaeleza kwamba lengo lao ilikuwa kwenda kutoa posa.

Alisema watuhumiwa hao walitaka kumpatia Miston Sh. 110,000 kama posa na mahari ambayo ilikuwa ng'ombe mmoja, mbuzi mmoja, blanketi moja na mashuka mawili.

Kamanda Kuzaga alisema jeshi hilo lilipata taarifa za siri na kwenda katika eneo hilo ambako lilishirikiana na viongozi wa kijiji akiwamo Mwenyekiti na Mtendaji wa kijiji kuwatia mbaroni watuhumiwa.

Alisema waliwakamata watuhumiwa wote watatu na kuwasweka ndani kwa ajili ya hatua mbalimbali za kisheria na kwamba walianza jitihada za kumsaka binti huyo.

Alisema watuhumiwa hao walihojiwa na wakaeleza alikokuwa amehifadhiwa binti huyo na kisha jeshi hilo likashirikiana na wananchi wa eneo hilo kumtafuta mpaka wakamkuta nyumbani kwa Chande.

Alisema jitihada za kumtafuta mtuhumiwa Chande Mwaigaga, ambaye alitorokea kusikojulikana zinaendelea na kwamba akipatikana ataunganishwa na watuhumiwa wanaoshikiliwa kwa ajili ya hatua za kisheria.

Kamanda Kuzaga, aliwataka vijana kuacha tabia ya kuwalaghai na kuwarubuni wanafunzi kitendo ambacho ni kinyume cha sheria na kinachosababisha kuwaharibia masomo.

Aidha, aliwataka wazazi na walezi kuacha kusaidia watoto wao katika vitendo vya uhalifu kwa maelezo kuwa watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Tatizo la wanafunzi wa kike kutoroka shule na kuolewa limeanza kuongezeka mkoani Mbeya, hivi karibuni aliyekuwa mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Panda Hill alitoroka na kuanza kuishi na mchoma mkaa ajulikanaye kwa jina la Baba Jose.



Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde (kushoto), akiambatana na baadhi ya viongozi wa Mkoa wa Mbeya na maofisa wa wizara hiyo kukagua teknolojia mbalimbali za kilimo zinazoonyeshwa kwenye maonyesho ya kimataifa ya kilimo (Nanenane) yanayofanyika Uwanja wa John Mwakangale jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Wananchi waanza kupata maji waliyokosa muda mrefu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SIKU chache baada ya Kamati ya Siasa ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mbeya, kutembelea Mradi wa Maji wa Bwawa la Matwiga, wilayani Chunya na kuiagiza serikali kushughulikia uhaba uliopo, tayari wananchi wameanza kupata huduma katika maeneo yote ya mradi.

Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji na usafi wa Mazingira vijijini (RUWASA), Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Hans Patrick, jana alisema vituo vyote vilivyokuwa vinatakiwa kutoa maji kwenye mradi huo tayari wananchi wanapata huduma.

Alisema wakati kamati ya siasa inapita wiki iliyopita ni vituo vitano pekee kati ya 17 ndivyo vilikuwa vinatoa huduma, lakini kwa sasa vituo vyote vinatoa maji.

Alisema mradi huo kwa sasa unahudumia vijiji viwili ambavyo ni Matwiga na Isangawana na kwamba wanaendelea kurekebisha maeneo ambayo huduma haipatikani kama ilivyokusudiwa na serikali.

"Nimekagua vituo vyote 17, nilikuwa nakagua kituo kimoja baada ya kingine na sasa huduma inapatikana vizuri na wananchi wanafurahia, tunashukuru Kamati ya Siasa ilitusaidia kubaini matatizo," alisema Injinia Hans. Alisema miradi yote ya RUWASA ambayo kamati ilitembelea wanaendelea na taratibu za kuhakikisha inakamilika na wananchi wanaanza kupata huduma.

Vilevile, alisema wanakusudia kuuhamisha mtambo huo kwenda wilayani Kyela ambako utatumika kuchoronga kisima kwenye shule ya wasichana ambayo imeanza kujengwa.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo alisema mtambo wa kuchoronga visima ukishahamishwa wilayani Chunya hautarudi hadi umalize kazi kwenye halmashauri zingine.

Alisema Wilaya ya Mbarali pia inakabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa maji na hivyo mtambo huo unatakiwa ukimaliza kazi Chunya uhamishiwe Mbarali.

# Halmashauri yajenga shule kumuenzi Prof. Mwandosya

**Na Nebart Msokwa,** BUSOKELO

HALMASHAURI ya Busokelo katika Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, imejenga shule mpya ya msingi na kuibatiza jina la Prof. Mark Mwandosya, ikiwa ni namna ya kumuenzi kutokana na mchango wake kwenye maendeleo ya halmashauri hiyo na taifa.

Shule hiyo imejengwa katika Mji wa Lwangwa yalipo Makao Makuu ya Halmashauri hiyo na inatarajiwa kuhudumia kata za Lwangwa na Kabula.

Shule hiyo imepewa jina hilo la Prof. Mwandosya baada ushauri wa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo, wakati wa ziara ya kukagua miradi ya maendeleo.

Dk. Mwakajumilo, alisema alifanya ziara katika wilaya nzima ya Rungwe ambayo Prof. Mwandosya, aliitumikia kwa muda mrefu, lakini hakuona mradi wowote uliopewa jina lake kama namna ya kutambua mchango wake.

Alisema ili kumuenzi ni vyema mradi wowote wa maendeleo ukapewa jina lake ili hata vizazi vijavyo vikumbuke na kutambua mchango wake.

"Miongoni mwa watu waliotoa mchango mkubwa wa maendeleo kwenye wilaya hii huwezi ukamwacha Prof. Mwandosya, amekuwa na mchango mkubwa ndani ya wilaya yetu na taifa, kwa hiyo nawashauri tafuteni namna ya kuuenzi huo mchango," alisema Dk. Mwakajumilo.

Juzi Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jaffar Haniu, alisema waliamua kuipa shule hiyo mpya jina la Prof. Mwandosya, kutokana na kwamba ndiyo shule mpya pekee ndani ya halmashauri hiyo.

Alisema shule hiyo ilikuwa bado haijasajiliwa na wala haijapewa jina na hivyo baada ya kushauriwa na Dk. Mwakajumilo wakaamua isajiliwe kwa jina hilo.

Ofisa Elimu Msingi na Awali wa Halmashauri ya Busokelo, Mwalimu Atuvonwe Chaula, alisema shule hiyo imejengwa kwa kutumia fedha za mradi wa BUST ambao unalenga kuongeza vyumba vya madarasa kwenye shule zenye idadi kubwa ya wanafunzi.

Alisema ujenzi wake umegharimu zaidi ya Sh. milioni 200 na ina majengo saba ambayo yana zaidi ya vyumba 14 ambavyo vitakuwa ni madarasa na ofisi za walimu.

Alisema Shule ya Msingi Lwangwa, ilikuwa imeelemewa na idadi kubwa ya wanafunzi kwa maelezo kuwa ina zaidi ya wanafunzi 800 jambo ambalo lilikuwa linawafanya wabanane kwenye vyuma vya madarasa.

"Halmashauri nzima tuliletewa zaidi ya Sh. milioni 600 kwa ajili ya mradi wa BUST, lakini fedha nyingi tulizielekeza kwenye hii shule mpya kwa sababu ya msongamano wa wanafunzi kwenye shule mama," alisema Mwalimu Chaula.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Busokelo, Loema Peter, alisema mradi huo umetekelezwa kwa kutumia mfumo wa akaunti ya dharura (Force account) ambao unataka kutumia mafundi wa mtaani.

Alisema shule hiyo walianza kuijenga Mei, mwaka huu na sasa inaelekea kukamilika na kwamba kazi zilizobaki ni za umaliziaji huku baadhi ya madarasa yakiwa yameshakamilika.

Prof. Mark Mwandosya, alitumikia Wilaya ya Rungwe, kama Mbunge wa Jimbo la Rungwe Mashariki ambalo kwa sasa linaitwa Busokelo na alikuwa Waziri kwenye wizara mbalimbali kabla ya kustaafu mwaka 2015.



# Serikali yafungua maeneo mapya utafutaji mafuta

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imefungua maeneo mapya ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia visiwani humo.

Ufunguzi huo unafungua awamu mpya ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia ambao una lengo la kukuza sekta hiyo, kwa kufungua fursa kwa wawekezaji wa utafutaji na uchimbaji wa nishati hiyo kuomba maeneo hayo kupitia zabuni ya kimataifa itakayotangazwa kabla ya kumalizika kwa mwaka 2023.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake mjini hapa, Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Masoud Suleiman Makame, alisema serikali inazikaribisha kampuni za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kuangalia data za Zanzibar na kuanza kupendekeza maeneo yanayowavutia zaidi katika kuwekeza kabla ya kuanza kwa zabuni hiyo.

"Zabuni hii ni zabuni ya kwanza kwa Zanzibar katika masuala ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia ikiwa ni moja ya shughuli katika mpango wa miaka mitano wa uendelezaji wa sekta hii hapa Zanzibar," alisema.

Masoud alisema chini ya uongozi wa Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, Zanzibar inaendelea kuwa kituo kikubwa cha uwekezaji kwa ajili ya kukuza na kuimarisha uchumi kwa maslahi ya wananchi wake.

"Hatua tuliyofikia leo ni ushuhuda wa uongozi wake imara na maono yake makubwa ambapo leo hii Zanzibar imeandika historia mpya ya kufanikisha ugawaji wa vitalu vipya na kuandaa zabuni ya kwanza ya utoaji wa vitalu kwa ajili ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia," alisema.

Aidha, alihakikishia kampuni za utafutaji na uchimbaji wa mafutaji na gesi asilia pamoja na wawekezaji kuwa milango iko wazi kwa ajili ya kuwapokea na wanatarajia ushirikiano mzuri na ushiriki wao katika sekta hiyo kwa kuwa karibu na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi asilia Zanzibar (ZPRA).

Alisema taarifa zote za mafuta na gesi zimekamilika kuchakatwa na kampuni ya Schlumberget na Serikali ya Zanzibar ilikabidhiwa na kampuni ya PUMA pamoja na TPDC za Dar-es-Salaam.

Waziri Makame alisema, Zanzibar ipo huru kufanya kazi za uchimbaji wa mafuta na gesi pamoja na shughuli zote za utafiti na hakuna vikwazo.

Alisema kazi za utafiti wa mafuta na gesi kwa muda mrefu zilifanywa na kampuni ya Rakgas katika hatua mbalimbali kabla ya kutokea tofauti na kushindwa kufuata masharti.

Makame alitoa ufafanuzi huo baada ya baadhi ya wanasiasa kudai kwamba Zanzibar haina uwezo wa kisheria wa kutoa leseni katika kazi za uchimbaji wa mafuta kwa sababu suala hilo ni miongoni mwa mambo ya Muungano.

"Nataka niwaambie wananchi na wawekezaji kwa ujumla kwamba hakuna vikwazo kwa Zanzibar kisheria kuchimba mafuta na gesi kwani kazi za aina hiyo tayari zimefanyika awali...suala la mafuta na gesi tayari limepatiwa ufumbuzi wake." alisema.

Hata hivyo, hakuvitaja vitalu vitakavyohusika na uwekezaji katika kutafuta mafuta na gesi na kudai kwamba ni siri na hayo ni makubaliano kati ya mwekezaji na wizara.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Utafiti na Uchimbaji wa Mafuta (ZPRA), Ali Khalil Mirza, alisema hiyo ni hatua nzuri ya kuifungua Zanzibar katika masuala ya utafiti na uwekezaji katika nishati ya mafuta na gesi.

"Haya ni mabadiliko makubwa ambayo sasa yanakwenda kuifungua Zanzibar katika sekta ya uwekezaji wa mafuta na gesi," alisema.



Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha ACT Wazalendo, Ismai Jussa Ladhu akihutubia mkutano wa hadhara wa chama hicho, katika uwanja wa Chwaka, Mkoa wa Kusini Unguja juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mwanakwerekwe wapongezwa kujenga kituo cha ujasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla, amepongeza hatua ya viongozi wa Jimbo la Mwanakwerekwe kujenga kituo cha wajasiriamali ili kuwasaidia vijana kupata ujuzi na kujikimu kimaisha.

Hemed aliyasema hayo wakati alipotembelea kituo hicho ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kukagua uhai wa chama katika majimbo yote ya uchaguzi ya Zanzibar.

Alisema kuwapo kwa kituo hicho kuna unga mkono dhamira ya Rais wa Zanzibar kuwawekea mazingira mazuri wajasiriamali.

Alisema kituo hicho kinasaidia kuwapatia ujuzi vijana wa jimbo hilo na wengine na hatimaye kuzalisha ajira nyingi zitakazowanufaisha vijana wa Zanzibar.

Akitoa taarifa ya Kituo cha Ujasiriamali Jimbo la Mwanakwerekwe, Katibu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, Said Saleh Said, alisema kituo hicho kimeanza rasmi mwaka 2022 kikiwa na lengo la kuwapatia elimu ya ujasiriamali vijana ili waweze kujiajiri na kujikimu kimaisha na kuondokana na mawazo potofu ya kujihusisha na vikundi viovu.

Alisema toka kuanzishwa kwa kituo hicho kimezalisha vijana wenye taaluma na uweledi mkubwa kwa kuzalisha bidhaa zilizo bora na zenye viwango pamoja na kuanzisha kitengo cha TEHAMA kwa ajili ya kutoa elimu ya habari na mawasiliano.

**Alisema kuwapo kwa kituo hicho kuna unga mkono dhamira ya Rais wa Zanzibar kuwawekea mazingira mazuri wajasiriamali.**

# Jeshi la Polisi latakiwa kuimarisha doria, huduma bora

**Na Mwandishi Wetu**

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, amewataka askari wa Jeshi la Polisi kuimarisha doria na kutoa huduma bora kwa jamii wakati wanapotekeleza majukumu yao ya kazi.

Aliyasema hayo huko Mkoa wa Kaskazini Unguja alipokua akizungumza na askari wa mkoa huo katika kikao kazi cha tathmini ya utendaji kazi wa Jeshi la Polisi. Kamishna Hamad alisema utoaji wa huduma bora kwa jamii utasaidia wananchi kuwa na imani na Jeshi hilo na kuunga mkono jitihada za serikali katika kukuza utalii na uwekezaji nchini.

"Serikali zetu zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimekuwa zikitangaza fursa za kiuchumi kwa wawekezaji na za kitalii ili kukuza uchumi wa nchi yetu kutokana na amani iliyopo na wananchi wana matarajio makubwa kwa Jeshi letu," alisema Kamishna Hamad.

Aliwasisitiza askari kutumia dhana ya polisi jamii kwa kuwapa elimu wananchi umuhimu wa utalii na kujiepusha na vitendo vya kihalifu kwa wageni na jamii kwa ujumla.

Aliwataka askari hao kuzingatia haki za binadamu wanapotoa huduma kwa wananchi wanapofika katika vituo vya polisi.

"Suala la kuzingatia haki za binadamu kwa askari wa Jeshi la Polisi wa cheo chochote kile sio hiari ni lazima na unapaswa uwahudumie wananchi kama unavyohitaji kuhudumiwa wewe unapoenda katika maeneo ya kijamii kama vile hospitali kufuata huduma na atakae tenda kinyume na hayo tutamchukulia hatua," alisema.

Kamishna Hamad alisema suala la udhalilishaji katika jamii ni changamoto licha ya Jeshi la Polisi kufanya bidii ikiwamo kutoa elimu kwa wananchi.

Alizitaja changamoto hizo kuwa ni pamoja na wananchi kushindwa kutoa ushirikiano wakati wa kukusanya upelelezi, kuchelewa kuripoti matukio hayo katika vituo vya polisi kwa wakati, mahali, ukosefu wa malezi bora na baadhi ya wanajamii kuliona suala la kuzuia vitendo vya udhalilishaji linawahusu polisi pekee.

"Jeshi la Polisi limekua likifanya doria, lakini doria hizi haziwezi kuzuia vitendo vya udhalilishaji kwani vitendo hivyo hufanyika katika maeneo ya vificho ambapo polisi hawapo, hivyo suala hili pia linahitaji doria za kiroho kwa waumini wa dini zote," alisema.

Kamada wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja, Kamishna Msaidizi, Daniel Shila, alisema hali ya usalama katika mkoa huo ni nzuri na wamejipanga kuendelea kuzuia na kutatua changamoto ya uhalifu na wahalifu na kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kujiepusha na kufanya vitendo vya kihalifu kwa wageni wanaofika nchini na katika jamii.

"Jeshi la Polisi limepeleka askari wenye cheo cha Mkaguzi katika kila shehia kutoa elimu na kushirikiana na wananchi kutatua changamoto za kihalifu zilizomo katika shehia zao," alisema.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Temeke**
**Kituo cha Jumuishi**
**Mkoa Dar es salaam**
**Usimamizi wa mirathi Na 904 /2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU JUMA MUSTAFA MAWENGE wa Mbezi Beach**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA ZUBEDA MGANGA MAWENGE**
**KADOGONDA MUSTAFA MAWENGE**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa mirathi Mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe……mwezi…mwaka…kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemuanaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 19 mwezi 06 mwaka 2023

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BAKHITA MATHIAS MANGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NEW HOLLAND** yenye usajili namba: **T691 CHG,** CHASSIS NAMBA: **1230109** na ENGINE NAMBA: **104527N.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**ARU/ARU/RB/213589/2023**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**NAJIM SHABANI MAKONGORO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya BOXER yenye namba za usajili MC442CSP. Chassis No. MD2A21BXXLWF92410, Engine No. PFXWLF20278. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DOD/DOD/RB/201870/2022.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 20 LA 2023**

**HADIJA IBRAHIM MUSSA MWOMBAJI/ WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**(1) DEO, (2) JAMES PETER (3) UMMY ABDALLAH MTONI MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**(1) DEO, (2) JAMES PETER (3) UMMY ABDALLAH MTONI**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

HADIJA IBRAHIM MUSSA amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (mwananyamala) shauri husika limepangwa kutajwa hukumu tarehe 11/09/2023 saa 3:00 Asubuhi mbele ya Mh J.W.SILLAS vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masijala ya wazi Baraza la Ardhi na Nyumba Kinondoni. Endapo hautatekeleza haya, Shauri litasikilizwa upande mmoja na Hukumu kutolewa.
Imetolewa na kutiwa saini na mhuri wa Baraza hili leo tarehe 31 Mwezi 07,2023

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT**
**AT MUSOMA**
**CIVIL CASE NO 07 OF 2023**
**MILELE ALPHONSO MUNDEBA……PLAINTIFF**
**VERSUS**
**STEPHEN JOSEPH MASELE…..DEFENDANT**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(ORDER V, RULE 1CPC)**

**TO : STEPHEN JOSEPH MASELE**
**P.O.BOX 455, GEITA.**
**PHONE NO : 0752 – 699 942**

**TAKE NOTICE THAT** THE PLAINTIFF HAS FILED THE SUIT AGAINST YOU, THE PARTICULARS OF THE CLAIMS ARE SET FORTH IN THE COPY OF THE PLAIN IN THE COURT.
YOU ARE HEREBY NOTIFIED UPON READING OF THE SUMMONS YOU MUST APPEAR IN THE COURT ON THE 14TH , AUGUST, 2023 AT 08:30 AM IN THE FORENOON AND FILE YOUR WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE WITHIN 21 DAYS FROM THE DATE OF PUBLICATION OF THE NOTICE/SUMMONS.
AND TAKE NOTICE FURTHER THAT IF YOU DEFAULT IN FILLING OF THE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE WITHIN SPECIFIED HEREINABOVE THE COURT MAY PRONOUNCE JUDGEMENT/RULING AGAINST YOU.
GIVEN UNDER MY HAND AMD SEAL OF THE COURT THIS 28TH, JULY, 2023.

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
MUSOMA/MARA

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

**ELISHA JAMES ISSANJA** anatangaza kupotea kwa kadi za magari zenye usajili namba : T 659 AKW, T 746 ANT, T 463 ABP na T 346 DKY. Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA :
**ARU/ARU/RB/257965/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



**AUJEN WILLIBARD** anatangaza kupotelewa na vyeti, cheti cha chakuhitimu kidato cha nne index **No. S.0676-0047 MABIRA SECONDARY SHOOL** mwaka 2014, na Kidato cha Sita index No. **S0150-0578 SAME SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017, Vilivyotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa. Cheti cha chuo chenye namba **003-0003189** pamoja na Transcript vilivyotolewa na **ST. JOHN'S UNIVERSITY OF TANZANIA** Mwaka 2021. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa polisi: **KAG/ RB/5017/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU COSTANTINE KIZWALO** MSINGI AMEPOTEZA KADI YAKE YA GARI AINA YA **TOYOTA RAV4** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T159 ARS.** KWA YEYOTE ATAKAEIONA AU KUOKOTA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI
**MAS/TR/RB/37/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**
**Kituo cha MJINI**
**Mkoa wa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 73/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**JOHN EDIMOND LYIMO wa MANZESE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUWATEUA WASIMAMIZI WAWILI YALIYOLETWA NA 1. ANGELINA JOHN LYIMO.**
**2. SHABANI ABDALLAH MWAWILA.**

**TANGAZO**
***(kanuni ya 5 (2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Maha kama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe **11** Mwezi **08** mwaka **2023** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia:** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa

* Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia *Futa isiyohusika

Imetolewa leo tarehe 27 mwezi 07 mwaka 2023

**IN THE HIGH COURT OF FTHE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA)**
**AT ARUSHA**
**LAND APPEAL NO. 123 OF 2022**
**(Original Application No. 121 of 2020 District Land and Housing Tribunal for Arusha at Arusha )**
**LORIVI TIRA KAMBEI……………APPELLANT**
**VERSUS**
**NMB BANK PLC……………………1ST RESPONDENT**
**KILICRAAS ADVENTURE &SAFARI AUCTIONEERS………2ND RESPONDENT**
**JOSEPH TOBIKO MOLLEL………………3RD RESPPONDENT**
**JOSEPH LELO MFOI………………4TH RESPONDENT**
**NOTICE OF MENTION**

**TO:**
- **NMB BANK PLS**
- **KILICRAAS ADVENTURE & SAFARI AUCTIONEERS**
- **JOSEPH TOBIKO MOLLEL**
- **JOSEPH LELO MFOI**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High court of Tanzania at Arusha on 15th day of AUGUST 2023 at 09:30a.m in the forenoon. You are required to appear in person.
TAKE FURTHER NOTICE THAT in default of your appearance on that day and time for mention , the court may proceed in your absence.
GIVEN under my HAND and SEAL of the COURT this 20th day of JULAY 2023

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT
ARUSHA

## TAARIFA KWA UMMA

Rejea tangazo la mnada wa hadhara la tarehe 29.07.2023 katika gazeti la Nipashe. Tunatoa taarifa kuwa jina la dalali lililosomeka DENNESTO INVESTMENT LTD liliandikwa kimakosa.

Jina sahihi lisomeke
DENNESTO COMPANY LIMITED

**Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335/0718276859**
**Dennesto Company Limited: 0658896226**

***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# CRDB yanyakua tuzo nne za kimataifa

**LAGOS,** NIGERIA

BENKI ya CRDB imenyakua tuzo nne za kimataifa za umahiri katika ugavi zijulikanazo kama Africa Procurement and Supply Chain Awards (APSCA) 2023 zilizotolewa jijini Lagos, Nigeria.

Benki yenyewe imeshinda tuzo mbili huku viongozi wake wakinyakua tuzo mbili kwa kutambua mchango wao katika kusimamia na kuongoza taratibu na viwango vya ununuzi na ugavi.

Katika hafla hiyo ya tuzo hizo, benki hiyo imenyakua tuzo ya umahiri katika ubunifu kwenye ununuzi na ugavi (sekta ya benki) na tuzo ya taasisi yenye idara bora ya ununuzi na ugavi.

Mkurugenzi Mtendaji wake, Abdulmajid Nsekela ametambuliwa kama Ofisa Mtendaji Mkuu Anayewezesha Vyema Idara ya Ununuzi na Ugavi huku Pendason Philemon, Mkurugenzi wa Ununuzi wa Benki ya CRDB akitunukiwa tuzo ya mchango mkubwa katika taaluma ya ununuzi na ugavi katika sekta ya benki akiwa miongoni mwa viongozi 50 wa eneo hilo waliotambuliwa katika awamu ya tano ya APSCA.

Akipokea tuzo kwa niaba ya Nsekela, Balozi wa Tanzania Nigeria, Dk. Benson Bana, alisema ni furaha kubwa kwake kuungana na Watanzania wenzake, hasa wafanyakazi wa Benki ya CRDB ambayo imeliheshimisha taifa kwa kushinda tuzo nne za umahiri katika ununuzi.

"Ninaipongeza sana Benki ya CRDB, viongozi na wafanyakazi wake hasa Bwana Abdulmajid Mussa Nsekela ambaye amepewa tuzo ya Ofisa Mtendaji Mkuu anayewezesha vyema Idara ya Ununzi na ndugu yangu Bwana Philemon ambaye amezawadiwa tuzo ya juu katika masuala ya ununuzi.

"Ni heshima kwa Watanzania, Benki ya CRDB imetuweka mbele na kutuheshimisha na imeendelea kuunga juhudi za Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan za kuifungua nchi kwa kuwa Tanzania sasa inasikika Nigeria na imesikika Afrika na sio kusikika tu bali pia kuzoa tuzo katika eneo la ununuzi kimataifa," alipongeza Balozi Bana.

Tuzo za APSCA huwatambua wataalamu, idara na taasisi zenye umahiri, mchango au umakini mkubwa katika kuzingatia viwango vya hali ya juu katika ununuzi na ugavi kimataifa.

Akielezea ushindi huo, Philemon alisema kila mwaka APSCA hutoa tuzo hizo, lakini Benki ya CRDB imeshiriki kwa maara ya kwanza mwaka huu ambao umeshuhudia washiriki 83 wakichuana nayo na benki kuibuka kidedea.

"Ilikuwa furaha na fahari ya aina yake kwa benki yetu kuitwa jukwaani mara nne kwenda kupokea tuzo za umahiri mbele ya mamia ya wataalamu wa fani ununuzi na ugavi.

"Ulikuwa usiku mzuri kwa Benki ya CRDB na kampuni ya mawasiliano ya MTN ya Nigeria tuliong'ara zaidi kwa kupata tuzo nyingi, nne kila taasisi. Tuzo hizi zinadhihirisha uwezo mkubwa wa Watanzania kwamba tunaweza kushindana kimataifa na kutoka kimasomaso, hivyo tujielekeze kupambana na wenzetu kutoka kokote duniani," alisema Philemon.

Kwa upande wake, Nsekela alisema usimamizi wa ununuzi na ugavi ni suala nyeti ambalo ni zaidi ya kuhamisha bidhaa kutoka kwa muuzaji kwenda kwa mteja.

"Kuhakikisha utekelezaji wake unakuwa sawia, kunahitaji jicho makini la menejimenti. Bila idara imara ya ununuzi na ugavi, benki haiwezi kutoa huduma bora kwa wateja wake. Mchango wa idara hii unajenga msingi wa mafanikio ya benki katika maeneo mbalimbali.

"Nimefurahi kuona idara yetu ununuzi na ugavi pamoja na menejimenti yake ikitambuliwa kutokana na umahiri wake kwa kuzingatia kanuni zinazotakiwa na kukubalika duniani kote. Ninaahidi nitaendelea kuipa ushirikiano kadri itakavyohitajika," alisema Nsekela.

Mkurugenzi huyo alieleza kwamba Bara la Afrika kwa sasa linatekeleza mkataba wa eneo huru la biashara unaoruhusu biashara, bidhaa na huduma kufanyika bila mipaka na pia raia wa kiafrika kuvuka mipaka bila vikwazo, hivyo kufungua soko la zaidi ya watu bilioni 1.3.

"Ili kulihudumia kiushindani soko hili, kampuni na taasisi zinapaswa kufanya biashara na kutoa huduma kwa kuzingatia vigezo na viwango vya kimataifa.

"Benki ya CRDB inakusudia kutoa huduma zake kwa watu wengi katika soko hili kubwa. Hilo litafanikiwa kwa kuwa benki inajikita katika umahiri wa kutoa huduma viwango vya kimataifa. Tuzo hizi tulizoshinda ni uthibitisho kwamba huduma zetu ni za kiwango kikubwa zinazolenga kukidhi malengo na matarajio ya wateja wetu," alisisitiza Nsekela.

Kwa miaka minne mfululizo, tuzo za APSCA zilikuwa zinafanyika Ghana. Zikifanyika Nigeria mwaka huu, tuzo hizo zimeandaliwa kwa ushirikiano wa Taasisi ya Ununuzi na Usimamizi wa Ugavi (CISCM)), Taasisi ya Ununuzi na Ugavi Ghana (GIPS) na Chama cha Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Nigeria (APPON).



Balozi wa Tanzania nchini Nigeria, Dk. Benson Bana (katikati), akipokea tuzo ya Mkurugenzi Mtendaji Bora anayesaidia manunuzi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Benki ya CRBD, Abdulmajid Nsekela kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Instictwave, Akin Naphtal katika hafla ya Tuzo za Ugavi (APSCA), jijini Lagos jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Manunuzi wa Benki ya CRDB, Pendason Philemon. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MAPINDUZI NIGER

# Wanajeshi Mali, Burkina Faso watoa onyo la vita

**NIAMEY,** NIGER

VIKOSI vya kijeshi vya Burkina Faso na Mali, vimesema jaribio lolote la nguvu la kumrejesha madarakani Rais Mohamed Bazoum katika nchi jirani ya Niger litaonekana kama tangazo la vita dhidi yao.

Hii inafuatia tishio kutoka katika kambi ya kikanda kwamba "itachukua hatua zote" ikiwa Rais hatorejeshwa madarakani.

Bazoum anazuiliwa na viongozi wa mapinduzi ya Niger baada ya kuondolewa madarakani wiki iliyopita.

Eneo hilo ambalo limetishiwa na waasi wa Kiislamu, limeshuhudia mapinduzi kadhaa katika miaka ya hivi karibuni.

Burkina Faso na Mali zimekataa uhusiano na nchi za Magharibi, hasa ukoloni wa zamani wa Ufaransa, na kukumbatia ushirikiano mpya na Urusi.

Onyo lao linaashiria mabadiliko makubwa ambayo yanaweza kuzidisha hali tete katika eneo hilo.

Kauli hiyo ya pamoja inakuja wakati Rais wa Chad, Mahamat Idris Déby amekuwa Niger, akiongoza juhudi za upatanishi kwa niaba ya Jumuiya ya Afrika Magharibi (ECOWAS) ili kutatua mgogoro huo.

Katika taarifa yao ya pamoja, Burkina Faso na Mali zilitishia kwamba ikiwa ECOWAS itaingilia kijeshi, watajiondoa katika umoja huo na kwenda kumtetea jirani yao wa mashariki.

Walisema uingiliaji kati kama huo utakuwa mbaya na utavuruga utulivu. Niger, ambayo pia ni koloni la zamani la Ufaransa, imekuwa mshirika mkuu wa magharibi katika vita vya wapiganaji wa jihadi wenye itikadi kali.

Baada ya viongozi wa kijeshi wa Mali kuchagua kushirikiana na kundi la Wagner la mamluki wa Urusi mwaka 2021, badala ya kikosi cha Ufaransa cha kukabiliana na ugaidi, Paris iliondoa kituo chake cha operesheni katika eneo hilo hadi Niger.

Siku ya Jumapili, ECOWAS ilipatia wiki moja mamlaka ya kijeshi iwe imemrejesha madarakani rais aliyechaguliwa, ambaye amezuiliwa katika Ikulu ya Rais katika mji mkuu, Niamey.

Serikali ya Niger haijatoa maoni yoyote juu ya mahitaji hayo, lakini iliapa kulinda nchi dhidi ya "uchokozi" wowote wa madola ya kikanda au Magharibi.

Imeishutumu Ufaransa kwa kupanga kuingilia kijeshi. Ufaransa haikuthibitisha au kukanusha madai hayo.

**BBC**

## HABARI MICHEZO

# AZAM YATAKA DAKIKA 180 DHIDI YA AS VITA, BANDARI

**Na Saada Akida**

BAADA ya kurejea nchini juzi wakitokea kambini Tunisia, Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema anahitaji dakika 180 za kucheza mechi mbili za kirafiki kabla ya kuelekea Tanga kwenye michezo maalumu ya Ngao ya Jamii.

Kwenye mechi hizo za Ngao ya Jamii, Azam itacheza dhidi Yanga Agosti 9, na mshindi wa mechi hiyo atacheza fainali Agosti 13, mwaka huu na timu itakayoshinda kati ya Simba na Singida Fountain Gate FC.

Azam ambayo tayari imecheza mechi tatu za kirafiki ikiwa Tunisia, imepanga kupata nyingine mbili katika uwanja wake wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam, ambapo itacheza dhidi ya Bandari FC ya Mombasa, Kenya na AS Vita ya DR Congo, iliyopo hapa nchini kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Hashim Ibwe, alisema timu imerejea nchini ikitokea Tunisia na watacheza mechi mbili za kirafiki za kujipima kabla ya kuvaana na Yanga katika mchezo wa Ngao ya Jamii kwenye uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Alisema wamemaliza kambi salama na kwamba Kocha Mkuu, Dabo, amepata alichokitaka kwenye maandalizi yake na sasa wako tayari kwa mashindano.

"Kwa hizi siku chache tukiwa nyumbani (Azam Complex), tutacheza mechi mbili za kirafiki za kimataifa dhidi ya AS Vita na Bandari FC kutoka Mombasa, hii michezo ni kwa ajili ya kocha kujiridhisha kwa kazi yake.

"Kazi nzuri imefanyika kwa benchi la ufundi, kilichobaki sasa ni kwa wachezaji kukifanyia kazi kile walichokipata kutoka kwa makocha wao," alisema Ibwe.

Kuhusu hali ya beki Charles Manyama, aliyepata jeraha la mkono, alisema anaendelea vizuri na anafanya mazoezi mepesi ili aweze kukaa sawa na kurudi kuipambania timu yake.

## Kagera Sugar yamsajili Chirwa

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kagera Sugar imenasa saini ya straika wa zamani wa Yanga na Azam FC, Obrey Chirwa, akitokea Ihefu FC.

Taarifa iliyotolewa mapema wiki hii na klabu hiyo, imeeleza kuwa imemsajili staika huyo ambaye pia ana uwezo wa kucheza kama winga kwa mkataba wa miaka miwili.

"Tunapenda kuuthibitishia umma kuwa tumeingia mkataba wa miaka miwili na aliyekuwa mchezaji na mshambuliaji wa Klabu ya Ihefu inayoshiriki Ligi Kuu," ilisema taarifa hiyo.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Ally Masoud, alisema tayari wameshakamilisha idadi ya wachezaji 12 wapya ambao walihitaji kuwachukua kwa msimu huu, huku wakiwa wameacha wachezaji saba.

Baadhi ya wachezaji ambao wamewasajili ni Abiud Khaledy, Dickson Gidion, Ally Ng'azi, Cleophace Mkandala, Richadsong Ng'ondya na wengineo ambao bado hawajawekwa wazi.

Chirwa raia wa Zimbabwe, aliyeingia nchini mwaka 2016 akitokea FC Platinum ya nchini kwao na kujiunga na Yanga hadi 2018 kabla ya kutimkia nje ya nchi, lakini muda mfupi tu baadaye akarejea na kujiunga na Azam FC timu aliyoitumikia hadi 2021 alipokwenda kujiunga na Namungo kwa msimu mmoja, aliichezea Ihefu kwa msimu mmoja pia.

Wakati huo huo, timu hiyo imetoka sare ya bao 1-1 dhidi ya JKT Tanzania kwenye mechi ya kirafiki iliyochezwa juzi uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga.

Timu zote zipo kwenye harakati ya kujaribu vikosi vyao kabla ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2023/24 kuanza Agosti 15, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu, Masoud, kikosi cha Kagera Sugar kinatarajiwa kuondoka nchini leo kwenda Uganda kwa ajili ya mechi kadhaa za kirafiki nia ikiwa ni ile ile, kujianda na msimu mpya wa Ligi Kuu.




Kiungo wa Simba, Fabrice Ngoma, akipima afya kabla ya kikosi cha timu hiyo kuondoka kambini nchini Uturuki jana. Wachezaji wote wa timu hiyo walipimwa afya kabla ya kuanza safari ya kurejea nchini. **MPIGAPICHA WETU**

## Waamuzi Ligi Kuu wapigwa msasa

**Na Abdallah Mataka**

WAKATI msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/24 ukitarajiwa kuanza rasmi Agosti 15, mwaka huu, Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi nchini, Nassoro Hamduni, amesema wamejipanga kuhakikisha wanafanya vizuri zaidi ya misimu iliyopita.

Akizungumza na Nipashe jana, Hamduni alisema timu nzima ya waamuzi ipo tayari na inaendelea na mafunzo mbalimbali kulekea msimu mpya wa ligi hiyo.

"Maandalizi kwa ajili ya msimu mpya wa ligi yanaenda vizuri mpaka kufikia hivi sasa tunavyozungumza tupo darasani na waamuzi kwa ajili ya mafunzo ya marekebisho ya sheria.

Aidha, Hamduni alisema wamefanyia kazi mapungufu yote ambayo yalijitokeza msimu uliopita hivyo ana imani watafanya vizuri zaidi .

"Ni kweli msimu uliopita kulikuwa na changamoto nyingi, lakini tumefanya maboresho, tumejitahidi kurekebisha makosa yote ambayo yalileta changamoto, tumeyafanyia kazi na kuhakikisha msimu mpya tunaanza tukiwa wapya kabisa," alisema Hamduni nakuongeza:

## Singida FG kuwatoa nyota iliyowaficha leo

**Na Adam Fungamwango**

HUKU Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Pindi Chana, akitarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye Kilele cha Tamasha la Singida Big Day leo katika uwanja wa Liti, Singida. Klabu ya Singida Fountaine Gate, imesema itawaanika wachezaji wake wote wapya iliyowasiliji kwa msimu ujao wa mashindano kwani ilikuwa imewaficha kwa makusudi.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hussein Massanza, alisema jana kuwa leo kikosi chao kitacheza dhidi ya AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ndiyo siku mashabiki watapata fursa ya kuwaona wachezaji wao wapya wa ndani na nje ya nchi iliyowasajili kwani walifanya kazi kubwa kuwaficha ili kulinogesha tamasha hilo.

"Tunafurahi kuona kuwa muitikio umekuwa mkubwa sana, msimu uliopita tuliwatambulisha wachezaji kabla ya Singida Big Day, lakini safari hii tumewaficha labda ni mmoja tu anayejulikana, lakini wengi wataonekana kwenye kilele cha tamasha na tulifanya hivyo kwa makusudi ili kulipa umuhimu na thamani kwa sababu kila mtu, kila shabiki anataka kuona ni wachezaji gani tumewasajili," alisema Masanza.

## ZISIKUPITE

### BAYERN YAKOMAA NA KANE

KLABU ya Bayern Munich iko tayari kuvunja rekodi ya euro milioni 80 iliyoweka wakati ilipomnunua beki Mfaransa Lucas Hernandez mwenye umri wa miaka 27, ili kumsajili mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 30 kutoka Tottenham. **(Sky Sports)**

### OSIMHEN AWINDWA AL-HILAL

AL-Hilal imewasilisha ombi la euro milioni 140 kumnunua mshambuliaji wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 24. **(Sky Sports)**

### KESSIE AWINDWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur huenda wakatumia fedha itakayopatikana kutokana na mauzo ya Harry Kane kuwanunua kiungo wa kati wa Barcelona na Ivory Coast, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 26 na mlinzi wa Ufaransa, Clement Lenglet, 28. **(Mundo Deportivo)**

### JOHNSON KUMRITHI KANE

TOTTENHAM Hotspur pia inamfuatilia mshambuliaji wa Nottingham Forest na Wales, Brennan Johnson mwenye umri wa miaka 22, ambaye thamani yake ni pauni milioni 50, ikiwa Harry Kane atauzwa. **(Mail)**

### MBAPPE NA CHELSEA

MMILIKI mwenza wa Chelsea, Todd Boehly, anakabiliwa na ushindani kutoka kwa Barcelona katika kutoa mkataba wa mchezaji pamoja na fedha taslimu kwa Paris St-Germain kwa mshambuliaji wao wa miaka 24 wa Ufaransa, Kylian Mbappe. **(Independent)**

### LUKAKU. VLAHOVIC KUPISHANA

CHELSEA pia wanatafuta mpango wa kubadilishana wachezaji unaomhusisha mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, mwenye umri wa miaka 30 na mshambuliaji wa Juventus Mserbia Dusan Vlahovic, 23. **(Fabrizio Romano)**

### LAVIA AKOMALIWA LIVER

LIVERPOOL inatayarisha ofa iliyoboreshwa kwa kiungo wa kati wa Southampton na Ubelgiji, Romeo Lavia, mwenye thamani ya pauni milioni 50, huku Chelsea na Manchester United pia wakimtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19. **(Mail)**

### NYONI ATAKIWA LIVERPOOL

KLABU ya Liverpool pia inakaribia kukamilisha dili la kumsajili kiungo wa Leicester City na England, Trey Nyoni, 16. **(Mirror)**

### JAMES AOTA MBAWA

KLABU ya West Ham iko tayari kuachana na mpango wa kumsajili kiungo wa Southampton mwenye thamani ya pauni milioni 40, James Ward-Prowse baada ya ombi la pili kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kukataliwa. **(Guardian)**

### LOKONGA AWANIWA BURNLEY

KLABU ya Burnley ipo kwenye mazungumzo na Arsenal kuhusu mkataba wa mkopo wa msimu mzima kwa kiungo wa Ubelgiji, Albert Sambi Lokonga mwenye umri wa miaka 23, wakati Auston Trusty mweye miaka 24 pia anaweza kuondoka, huku Sheffield United ikiongoza mbio za kumnunua beki huyo wa Marekani. **(Telegraph)**

## DOND A SOKA MAGA ULAYA




# FABINHO ATUA RASMI AL-ITTIHAD YA SAUDIA

**Leo naondoka nyumbani kwangu, imekuwa miaka mitano nikivaa jezi hii na siku zote nikiwa na heshima kubwa...**

**JEDDAH, Saudi Arabia**

KIUNGO wa kati wa Brazil, Fabinho amejiunga na Al-Ittihad kutoka Liverpool kwa mkataba wa miaka mitatu, klabu hiyo ya Saudi imetangaza.

Taarifa za kifedha hazikuwekwa wazi, lakini vyombo vya habari vya England viliripoti kuwa mabingwa hao wa Saudi Pro League walilipa pauni milioni 40 kwa ajili ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29.

Al-Ittihad ilichapisha video kwenye ukurasa wa X (zamani Twitter) yenye kichwa cha habari "Chui wanaruhusiwa kupita" wakimaanisha ripoti za vyombo vya habari zinazopendekeza mpango huo ukacheleweshwa kwa sababu ya kuzaliana kwa mbwa wa Fabinho ambao wamepigwa marufuku kuingia Saudia.

Video hiyo ilimuonyesha kiungo huyo akiwa ameshikilia kamba ya Chui na kusema: "Mimi ni Chui."

"Leo naondoka nyumbani kwangu. Imekuwa miaka mitano nikivaa jezi hii na siku zote nikiwa na heshima kubwa."

Fabinho anajiunga na mshindi wa Ballon d'Or, Karim Benzema na mchezaji wa zamani wa Chelsea, N'Golo Kante katika klabu hiyo yenye maskani yake Jeddah.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil aliichezea Liverpool mechi 219 tangu alipowasili mwaka 2018, na aliisaidia timu hiyo kunyakua mataji ya Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa, Kombe la FA, Kombe la Ligi na UEFA Super.

Jordan Henderson pia aliondoka Liverpool wiki iliyopita na kujiunga na Al-Ettifaq ya Steven Gerrard ya Saudi Arabia.

Ligi ya Saudia Pro League imekuwa kivutio kwa wachezaji wa hadhi ya juu tangu Cristiano Ronaldo alipohamia Al-Nassr Januari mwaka jana katika mkataba ulioripotiwa kuwa na thamani ya karibu dola milioni 220.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,139,8

JACKPOT MECHI WIKI HII
TAREHE: 03 AGOSTI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/08/23 | 17:00 | Tobol Kostanay vs FC Basel | 3.10 | 3.40 | 2.16 |
| 02. 03/08/23 | 18:00 | Pyunik Yerevan vs Kalmar | 2.31 | 3.25 | 2.95 |
| 03. 03/08/23 | 18:00 | Santa Coloma vs Sutjeska | 2.80 | 3.40 | 2.33 |
| 04. 03/08/23 | 19:00 | Urartu vs Farul Constanta | 2.51 | 3.21 | 2.71 |
| 05. 03/08/23 | 19:00 | FK Panevezys vs Hapoel Beer Sheva | 3.06 | 3.36 | 2.20 |
| 06. 03/08/23 | 19:45 | Zalaegerszegi TE vs NK Osijek | 2.51 | 3.27 | 2.66 |
| 07. 03/08/23 | 20:00 | Sepsi Osk vs CSKA Sofia | 2.71 | 3.21 | 2.51 |
| 08. 03/08/23 | 20:00 | Dila Gori vs Vorskla Poltava | 2.35 | 3.35 | 2.80 |
| 09. 03/08/23 | 21:00 | Vojvodina vs Apoel Nicosia | 2.75 | 3.25 | 2.44 |
| 10. 03/08/23 | 21:00 | Aarhus vs Brugge | 3.10 | 3.25 | 2.22 |
| 11. 03/08/23 | 21:30 | Larne vs KF Ballkani | 2.65 | 3.39 | 2.46 |
| 12. 03/08/23 | 21:45 | FC Luzern vs Djurgardens IF | 2.11 | 3.40 | 3.20 |
| 13. 03/08/23 | 22:00 | Shamrock Rovers vs Ferencvaros TC | 3.05 | 3.30 | 2.23 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa · vodacom m-pesa · halopesa · airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# VAN DIJK NAHODHA MPYA LIVERPOOL



**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL imemteua Virgil van Dijk kama nahodha mpya wa klabu hiyo, huku beki mwenzake Trent Alexander-Arnold akichukua nafasi ya usaidizi, klabu hiyo ya Ligi Kuu England imetangaza.

Van Dijk, ambaye pia ni nahodha wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, atachukua nafasi ya Jordan Henderson baada ya kiungo huyo wa kati wa England kujiunga na klabu ya Saudi Pro League ya Al-Ettifaq wiki iliyopita, na kuhitimisha miaka 12 ya kukaa Anfield.

Van Dijk amecheza mechi 222 kwa wababe hao wa Merseyside tangu alipohamia kutoka Southampton mwaka 2018.

"Ni siku ya fahari sana kwangu, kwa mke wangu, kwa watoto wangu, familia yangu. Imekuwa hisia maalum na siwezi kuielezea kwa wakati huu. Lakini ni jambo ambalo ninajivunia sana, " alisema Van Dijk katika taarifa.

"Nitafanya kila niwezalo na kile ninachoweza kufanya ili kumfanya kila mtu ajivunie na kufurahi pamoja nami na klabu ya soka."

Baada ya kukosa nafasi ya kucheza mara nne msimu wa 2021-22, na kushinda mataji mawili ya nyumbani, Liverpool haitashiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza chini ya Jurgen Klopp tangu kocha huyo alipochukua mikoba ya ukocha msimu wa 2016-17.

"Pia tunapaswa kuwa na subira kidogo, lakini tunataka kuwa pale na tunataka kuonesha kile tunachoweza kwa sababu tuna kundi la wachezaji, wafanyakazi, mashabiki, " aliongeza Van Dijk.

"Yote ni juu ya kuifanya pamoja na uthabiti na tunatumaini kuwa tunaweza kuionyesha."

Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 24 alijiunga na akademi ya Liverpool mwaka 2004 na kuwa nahodha

# PSG wampeleka Mbappe Chelsea

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain inaendelea kumtoa Kylian Mbappe kwa klabu kote Ulaya, ikiwa ni pamoja na Chelsea, vyanzo vimeiambia 90min.

PSG wanataka kumuuza Mbappe msimu huu wa majira ya joto ili kuepuka kumpoteza bure mkataba wake utakapokamilika mwakani na wameweka wazi msimamo huo kwa nahodha huyo wa Ufaransa na wawakilishi wake.

Mabingwa hao wa Ligue 1 hivi majuzi walikubali dau la rekodi ya dunia la pauni milioni 300 kutoka kwa Al Hilal, lakini Mbappe mwenyewe alikataa.

Rais wa PSG, Nasser Al-Khelaifi ameweka wazi anataka kumuuza mchezaji huyo, inaaminika kwamba Mbappe mwenyewe anataka kwenda Real Madrid.

Real na Mbappe wote wamekanusha madai ya PSG kwamba dili lipo tayari.

Al-Khelaifi sasa amewasiliana na Chelsea na mmliki wa klabu hiyo, Todd Boehly kuhusu uwezekano wa kumsajili Mbappe ili kujaribu kuwasukuma watoe ofa.

Ingawa Chelsea itakuwa tayari kuwasili kwa fowadi huyo wa zamani wa Monaco, kama vile Liverpool na Manchester City, hakujakuwa na pendekezo kutoka kwa kambi ya mshindi huyo wa Kombe la Dunia la kutaka kuhamia England.

Mbappe aliweka wazi hadharani kuwa hashinikiza kuondoka msimu huu wa majira ya joto, badala yake aliiambia PSG kuwa atakataa sehemu yake ya chaguo la pande mbili ambalo lingeongeza mkataba wake kwa mwaka zaidi hadi 2025.

Uamuzi huo wa mapema msimu huu wa majira ya joto uliwakasirisha PSG, na kusababisha msimamo wao wa 'kuuza sasa' wakati wa dirisha la usajili.

PSG sasa wanajikuta wakiwa kwenye mvutano na Mbappe katika nafasi kubwa kwenye sakata la uhamisho.

Hawawezi kumlazimisha kwenda Al Hilal na bado hawajaweza kuwezesha kwenda Real Madrid au kwingineko msimu huu wa majira ya joto.

Ikiwa Mbappe ataamua kubakia PSG hadi 2024, hakuna chochote wanachoweza kufanya kuzuia hilo.

## HABARI MICHEZO


359,317/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 06/08/23 | 13:00 | Urawa Red Diamonds vs Yokohama Marinos | 2.23 | 3.35 | 2.70 |
| 02. 06/08/23 | 13:00 | Kyoto Sanga FC vs Kashiwa Reysol | 2.22 | 3.05 | 2.90 |
| 03. 06/08/23 | 13:00 | Sagan Tosu vs Avispa Fukuoka | 2.40 | 3.00 | 2.70 |
| 04. 06/08/23 | 13:00 | Thespakusatsu vs Tochigi SC | 2.75 | 2.90 | 2.45 |
| 05. 06/08/23 | 13:00 | Omiya Ardija vs Blaublitz Akita | 2.65 | 2.95 | 2.46 |
| 06. 06/08/23 | 13:00 | Tokushima Vortis vs JEF United Ichihara Chiba | 2.85 | 3.05 | 2.27 |
| 07. 06/08/23 | 14:30 | Karlsruher SC vs Hamburger SV | 2.90 | 3.70 | 2.16 |
| 08. 06/08/23 | 14:30 | 1 FC Nuremberg vs Hannover 96 | 2.16 | 3.55 | 3.00 |
| 09. 06/08/23 | 14:30 | RSC Anderlecht vs Royal Antwerp FC | 2.41 | 3.45 | 2.65 |
| 10. 06/08/23 | 16:00 | Kalmar FF vs AIK | 2.55 | 3.00 | 2.55 |
| 11. 06/08/23 | 16:00 | FK Teplice vs FK Jablonec | 2.60 | 3.20 | 2.37 |
| 12. 06/08/23 | 17:30 | Grasshopper Club Zurich vs FC Basel 1893 | 2.75 | 3.45 | 2.16 |
| 13. 06/08/23 | 18:00 | FK Haugesund vs Rosenborg BK | 2.75 | 3.25 | 2.23 |
| 14. 06/08/23 | 18:00 | Tromsoe IL vs Lillestrom SK | 2.27 | 3.25 | 2.70 |
| 15. 06/08/23 | 18:00 | Blau-Weiss Linz vs TSV Hartberg | 2.39 | 3.25 | 2.55 |
| 16. 06/08/23 | 19:00 | Sunderland AFC vs Ipswich Town | 2.46 | 3.30 | 2.70 |
| 17. 06/08/23 | 20:15 | KV Kortrijk vs St. Truidense VV | 2.80 | 3.40 | 2.33 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 02/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1251 | Nagoya Grampus vs Urawa Red Diamonds | 2.60 | 3.11 | 2.55 |
| 13:00 | 1264 | Kashiwa Reysol vs Consadole Sapporo | 2.80 | 3.46 | 2.21 |
| 13:00 | 1732 | Ventforet Kofu vs Vissel Kobe | 3.88 | 3.62 | 1.77 |
| 13:00 | 1856 | FC Tokyo vs Roasso Kumamoto | 2.15 | 3.21 | 3.10 |
| 13:00 | 4274 | Jamaica W vs Brazil W | 11.24 | 5.52 | 1.21 |
| 13:00 | 4615 | Kawasaki Frontale vs Kochi United SC | 1.24 | 5.49 | 8.95 |
| 13:00 | 5282 | Panama W vs France W | 20.33 | 9.55 | 1.06 |
| 13:00 | 5538 | Tochigi SC vs Avispa Fukuoka | 3.11 | 3.21 | 2.14 |
| 13:00 | 5948 | Cerezo Osaka vs Shonan Bellmare | 1.78 | 3.52 | 3.92 |
| 14:30 | 4295 | Bayern Munchen vs Liverpool | 2.36 | 3.82 | 2.41 |
| 17:00 | 4099 | Astana vs Dinamo Zagreb | 3.50 | 3.27 | 2.00 |
| 18:00 | 3962 | SK Prostejov vs Sparta Prague B | 2.00 | 3.38 | 3.18 |
| 18:00 | 4222 | Cittadella vs Vecomp Verona | 1.70 | 3.70 | 3.80 |
| 18:00 | 4796 | Loudoun United FC vs Memphis 901 FC | 3.21 | 3.61 | 1.95 |
| 18:30 | 1501 | Hps W vs HJK Helsinki W | 7.80 | 5.40 | 1.24 |
| 19:00 | 1590 | FK Viktoria Zizkov vs SK Lisen | 2.97 | 3.12 | 2.21 |
| 19:00 | 2182 | Zbrojovka Brno vs Dukla Prague | 1.78 | 3.48 | 3.84 |
| 19:00 | 3050 | Pribram vs Opava | 2.07 | 3.22 | 3.17 |
| 19:00 | 3464 | Vyskov vs Kromeriz | 1.63 | 3.84 | 4.25 |
| 19:00 | 4057 | Karabakh vs Rakow Czestochowa | 2.00 | 3.23 | 3.58 |
| 19:00 | 4312 | Varnsdorf vs Graffin Vlasim | 2.12 | 3.44 | 2.88 |
| 19:00 | 5182 | MFK Chrudim vs Taborsko | 2.12 | 3.19 | 3.09 |
| 19:00 | 5481 | Jihlava vs Sigma Olomouc B | 2.03 | 3.38 | 3.12 |
| 19:30 | 2326 | Lorient vs Nantes | 2.50 | 3.32 | 2.51 |
| 19:30 | 4907 | Napoli vs Girona | 1.49 | 3.95 | 5.20 |
| 20:00 | 1461 | Arsenal vs Monaco | 1.60 | 3.78 | 4.76 |
| 20:00 | 1592 | Molde vs HJK Helsinki | 1.20 | 5.76 | 11.91 |
| 20:00 | 1596 | Maccabi Haifa vs Sheriff Tiraspol | 1.40 | 4.17 | 7.35 |
| 20:00 | 2279 | BK Hacken vs KI Klaksvik | 1.27 | 5.35 | 8.72 |
| 20:00 | 2801 | Racing Genk vs Servette Geneva | 1.56 | 4.07 | 4.96 |
| 20:00 | 3111 | AEK Larnaca vs Torpedo Zhodino | 1.31 | 5.20 | 8.01 |
| 20:30 | 3120 | Dudelange vs Gzira United | 1.51 | 3.94 | 6.18 |
| 21:00 | 3301 | FC Jarfalla vs Enskede IK | 2.75 | 3.72 | 2.14 |
| 21:00 | 3334 | UMF Grindavik vs IF Vestri | 2.41 | 3.38 | 2.51 |
| 21:00 | 4338 | Vidir vs Kari | 1.77 | 3.71 | 3.76 |
| 21:00 | 5132 | Augnablik vs Arbaer | 2.32 | 3.72 | 2.50 |
| 21:00 | 5451 | KF Fjallabyggd vs Throttur Vogum | 3.15 | 3.95 | 1.82 |
| 21:00 | 5532 | Thor Akureyri vs Fjolnir | 3.43 | 3.93 | 1.77 |
| 21:00 | 5593 | Copenhagen vs Breidablik | 1.25 | 5.38 | 9.36 |
| 21:30 | 1350 | Galatasaray vs Zalgiris | 1.14 | 6.67 | 16.24 |
| 21:30 | 2912 | Colon Santa Fe vs Lanus | 3.21 | 2.90 | 2.25 |
| 21:30 | 4109 | Gimnasia Y Tiro De Salta vs Central Norte Salta | 2.16 | 2.69 | 3.76 |
| 22:00 | 1579 | Santiago Morning vs San Luis Quillota | 2.49 | 3.06 | 2.70 |
| 22:15 | 1255 | Vikingur Olafsvik vs IR Reykjavik | 2.45 | 3.70 | 2.26 |
| 22:15 | 2181 | IA Akranes vs Leiknir | 1.71 | 4.05 | 3.59 |
| 22:15 | 2649 | Afturelding vs Grotta | 1.29 | 4.95 | 7.47 |
| 22:15 | 3443 | Haukar vs Hottur | 1.97 | 3.80 | 2.85 |
| 22:15 | 4573 | Ymir vs Magni | 2.71 | 3.32 | 2.33 |
| 22:15 | 4889 | Throttur Reykjavik vs Njarovik | 1.91 | 3.39 | 3.44 |
| 22:15 | 5614 | UMF Selfoss vs Aegir | 1.58 | 4.34 | 4.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# JKU KUJICHIMBIA MBWENI KUIWINDA SINGIDA FG CAF

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya JKU ya Zanzibar, inatarajia kuweka kambi jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujiandaa na mchezo wa Kombe la Shirikisho barani Afrika dhidi ya Singida Fountain Gate, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili mapema wiki hii kutoka visiwani Zanzibar, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Salum Ali, alisema kambi hiyo itaanza rasmi kesho na itakuwa JKT Mbweni, Dar es Salaam.

"Tutahamishia kambi yetu JKT Mbweni tukiwa na lengo la kufanya vema kwenye michezo yetu ya kimataifa," alisema Ali.

Alisema pia watapata nafasi ya kucheza mchezo wa kirafiki dhidi ya Azam FC na kwamba tarehe rasmi ya mchezo huo wataitangaza muda wowote.

Aliongeza kuwa maandalizi waliyoyafanya ikiwa ni pamoja na kucheza michezo miwili ya kirafiki, yamemsaidia kuona wapi pakuboresha zaidi huku akisifu viwango vilivyooneshwa na wachezaji wake.

Alisema ameamua kuhamishia kambi hiyo Dar es Salaam ili kuwawezesha wachezaji wake kuzoea mazingira pamoja na hali ya hewa kabla ya mchezo wao wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Singida Fountain Gate FC.

Kwa mujibu wa droo ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, mshindi wa jumla kati ya JKU na Singida Fountain Gate FC, atakutana na Future FC (Coca-Cola FC) ya Misri katika raundi ya pili na mshindi wa jumla atafuzu moja kwa moja hatua ya makundi ya kinayang'anyiro hicho kinachoshika nafasi ya pili kwa utajiri barani humu.

# Robertinho azitisha timu Ligi Kuu, CAF

INATOKA UK. 24

kwa nini?

"Lengo lilikuwa ni kutoa nafasi kwa wachezaji wote na kuona viwango vyao pamoja na utimamu wa miili yao ipo vizuri au vibaya," alisema.

Kikiwa nchini Uturuki kwa wiki tatu, kilicheza mechi nne dhidi ya Zira FC ya Azerbaijani na kutoka sare ya bao 1-1 na mara mbili dhidi ya Turan Tovuz ikishinda mabao 2-0, kabla ya kuchapwa bao 1-0 mechi ya pili jioni na kisha kuiadhibu Batman Petrol Spor ya nchini humo mabao 4-1, mechi zote zikichezwa Uwanja wa Soguksu Spor Kompleksi.

Katika hatua nyingine, kuelekea Simba Day, Jumapili wiki hii, ikiwa ni baada ya juzi usiku kuingiza Sh. milioni 29 kwa kupiga bei kibegi na jezi zilizokuwa zimebebwa ndani ya kibegi hicho kupandishwa mlima Kilimanjaro kwa ajili ya uzinduzi, klabu hiyo imezindua kampeni mpya ya kibegi itwayo 'Kibegi Part Two" ambapo ndani yake kukiwa na kitu kinaitwa 'Shabiki Bingwa'.

Kuelekea Kilele cha Siku ya Simba, juzi usiku Simba ilifanya mnada wa jezi hizo ambazo ziliandikwa majina ya viongozi wakuu wa nchi; Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais Philip Mpango, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson pamoja na rais wa Heshima na Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji, iliyouzwa kwa Sh. milioni mbili.

Inayofuata ilikuwa Jezi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Mwinyi ambayo imenunuliwa na HASA Clearing and forwarding kwa Tsh milioni 5.

Jezi ya Rais Samia iliuzwa kwa Sh. milioni 10, ikifuatiwa na ya Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi ambayo iliuzwa Sh. milioni 5 huku ya Makamu wa Rais Dk. Mpango ikiuzwa Sh. milioni 3 huku ile ya Waziri Mkuu, Majaliwa ikinunuliwa kwa Sh. milioni 4 na ya Spika, Dk. Tulia Sh. milioni 2.5 wakati kibegi kikinunuliwa kwa Sh. milioni 2.5

Akizungumza na Nipashe jana, Mtendaji Mkuu wa Simba, Iman Kajula alisema mbali na mnada huo pia siku hiyo maalum ya Agosti 6, mwaka huu, watakuwa na mnada mwingine wa kibegi na jezi.

Alisema tukio hilo litafanywa na wachezaji wote watakuwa wakifanya mnada wa moja ya jezi ya Simba na kigeni za raundi ya pili mbali na kile ambacho kimependa mlima Kilimanjaro.

"Jezi zote ambazo zimepigwa mnada leo (jana) zitatolewa kwa wahusika siku hiyo ya tamasha kwa kila mmoja kukabidhiwa na kwenye jezi kutakuwa na saini za watu ambao majina yao yako kwenye uzi huo uliopanda mlima Kilimanjaro.

"Tunahitaji kuiboresha ICU ya mama na watoto wachanga, vifaa vya kinamama kwa ajili ya kujiandaa kabla ya kujifungua na kina baba kushuhudia watoto wao wanapozaliwa, kabla ya mama kutoka chumba cha kujifungulia," alisema Kajula.

**UZINDUZI WA KUELEKEA SIMBA DAY:**

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu alisema wamefanya usajili mzuri kwa wachezaji kwa ajili ya kufikia malengo yao ya kutwaa mataji kwa msimu wa 2023

"Tumeandika barua kupeleka Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kuomba kutumia uwanja wa Uhuru kwa ajili ya kufunga Television kubwa na mashabiki waliokosa tiketi kuingia bure kushuhudia sherehe kubwa ya utambulisho wa usajili wa wachezaji wapya na kuona kikosi cha msimu mpya wa 2023/24," alisema Mangungu.

Meneja Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema kutakuwa awamu ya pili ya Kibegi ambacho kitajulika kama 'Shabiki Bingwa' ndani yake kutakuwa na tiketi 20 za Platinum kwa ajili mashabiki 20 ambao watakaa katika sehemu maalum kwa ajili ya kukaa na viongozi mashuhuri watakaokuwapo siku hiyo.

# 'Yanga itaonekana Ngao ya Jamii'


Gamondi

INATOKA UK. 24

Kocha huyo raia wa Argentina, alisema lengo kuu la benchi lake la ufundi msimu huu ni kuhakikisha timu inafanya vizuri zaidi ya msimu uliopita ambao Yanga ilifanikiwa kucheza fainali ya Kombe la ShirikishoAfrika lakini pia ilitetea ubingwa wake wa Ligi Kuu na Kombe la FA.

# Michezo

Jumatano Agosti 2, 2023

Nipashe




## Fabinho atua Al-Ittihad ya Saudia

UKURASA 21

TUPO TAYARI...



Wachezaji wa Simba wakianza safari Uturuki ya kurejea nchini jana. Kikosi hicho kilikuwa kimeweka kambi ya wiki tatu nchini humo kimerejea leo alfajiri tayari kwa sherehe za Simba Day Jumapili wiki hii na baadaye Ngao ya Jamii, kabla ya kuanza mikikimikiki ya Ligi Kuu Bara itakayoanza Agosti 15, mwaka huu. **PICHA: SIMBA**

# ROBERTINHO AZITISHA TIMU ZA LIGI KUU, CAF

●●●Aanika mbinu zake akisema ni kujenga kambi langoni mwao, Simba nayo yazindua kampeni mpya ya kibegi...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Simba kikirejea nchini leo alfajiri kutokea Uturuki kilipoweka kambi ya kujiandaa na msimu mpya wa mashindano, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbrazili Roberto Oliveira amesema msimu unaokuja wapinzani wake watakuwa na tabu sana kwa sababu ameandaa kikosi kitakachokuwa kinashambulia tu mfululizo bila kupaki basi.

Simba inayoshika nafasi ya tisa kwa ubora barani Afrika, iliweka kambi Uturuki kujiandaa na msimu mpya wa mashindano; Ligi Kuu Bara, Kombe la FA, Ligi ya Mabingwa Afrika na michuano ya African Football League (Super Liague) itakayoshirikisha timu bora 10 barani Afrika.

Akizungumza nchini Uturuki wakati timu ikijiandaa kurejea, kocha huyo alisema tayari ameshapata kikosi alichokuwa akikihitaji, sasa kazi ni moja tu kucheza soka ambalo yeye analipenda, ambalo ni la kumshambulia mpinzani na kutompa pumzi ya kutoka langoni mwake kwa dakika zote 90.

Alisema kutokana na aina hiyo ya soka kazi aliyokuwa akiifanya ni kuhakikisha wachezaji wake wanakuwa na utimamu wa mwili na pumzi ili kuweza kutekeleza vizuri majukumu hayo.

"Sipendi mtindo wa kukaa nyuma na kujilinda eti kikubwa ni alama tatu, huo si mtindo wa uchezaji wangu au falsafa ya Simba, napenda zaidi wachezaji wanaocheza kwenye eneo la mwisho la uwanja, narudia hata wapinzani wakisikiliza hakuna shida, narudia tena, napenda kucheza kwenye eneo la mwisho la uwanja la mpinzani," alisisitiza kocha huyo.

Akiizungumzia 'pre season', alisema ilikuwa ya mafanikio ingawa alisema baadhi ya wachezaji hasa waliokuja mwishoni bado hawajawa na utimamu wa mwili anaouhitaji, lakini atalifanyia kazi timu itakapokuwa hapa nchini.

"Kwa sasa nina machaguo mengi kuliko msimu uliopita, lakini tunahitaji muda kwa sababu tuna makundi mawili, kundi la kikosi cha kwanza wapo tayari, lakini kundi la pili linahitaji muda wa mazoezi ya viungo na ufundi na baada ya hapo mazoezi ya mbinu, unakumbuka niliandaa mechi mbili za kirafiki katika siku moja, unajua ni

UKURASA. 23

## Gamondi: Yanga rasmi itaonekana Ngao ya Jamii

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamond amesema mashabiki wa klabu hiyo watarajie mabadiliko chanya ya kiuchezaji ambayo yataanza kuonekana kwenye michezo ya Ngao ya Jamii.

Yanga itacheza na Azam FC Agosti 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani ikiwa ni mchezo wa kwanza na mshindi atacheza na timu itakayoshinda katika mchezo mwingine utakaozikutanisha Simba dhidi ya Singida Fountain Gate FC kuwania Ngao ya Jamii kwa msimu wa 2023/2024.

Gamondi ambaye anaendelea kuiandaa timu hiyo kwenye kambi yao waliyoiweka Avic Town, Kigamboni Dar es Salaam, alisema baada ya mchezo wao wa kwanza wa kirafiki kwenye Kilele cha Siku ya Mwananchi dhidi ya Kaizer Chiefs, ameendelea kuiongezea makali timu hiyo na kwa sasa wamezidi kuimarika kuelekea kwenye msimu mpya wa mashindano watakayoshiriki.

Alisema mchezo wa kuwania Ngao ya Jamii watakaoanza kucheza Agosti 9, utatoa picha kamili ya kikosi chake na mashabiki wataona mfumo wake wa uchezaji.

"Tunaendelea na program zetu za mazoezi, nafurahishwa na namna wachezaji wangu wanavyojituma na walivyo wepesi kushika maekekezo yangu, tuna mchezo wa Ngao ya Jamii kabla ya kuanza kwa Ligi Kuu, naamini mchezo huo utatoa picha kamili ya kikosi changu namna kilivyobadilika kucheza," alisema Gamondi.

Alisema anatarajia kucheza mchezo mwingine wa kirafiki kabla ya kwenda Tanga kwenye mchezo huo wa Ngao ya Jamii.

"Nadhani mchezo mwingine wa kirafiki utatuweka sawa tayari kwa mechi ya kuwania Ngao ya Jamii, kwa muda mfupi niliokuwa na timu nimeona ina mashabiki wengi wenye kiu ya mafanikio, naomba waendelee kuisapoti timu yao kwenye michezo ya mashindano yote ambayo tutashiriki," alisema Gamondi.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >